# MOFOFONOLOJIA YA MANENO MKOPO YA KIARROR KUTOKA KISWAHILI

**YEGO MERCY JEPKEMBOI**

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2022**

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa na mtu yeyote kwa madhumuni ya kutosheleza mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.

Sahihi…………………………………………… Tarehe 16 | 11 | 2022…………………………………...

YEGO MERCY JEPKEMBOI

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi

Sahihi………………………………………… Tarehe 16/11/2022…………………………………..

DKT. BASILIO MUNGANIA

Sahi…………………………………………..Tarehe 17/11/2022………………………………..

DKT. PRISCAH JERONO

## TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa:

Mume wangu:

Bobson Kambale Shihugwa

Wanangu:

Mark Robert Shihugwa

Donatta Wakesho Shihugwa

Melissa Akakhala Shihugwa

Wazazi wangu:

Erick Yego Kisoi na Priscah Kobilo Yego.

# SHUKRANI

Kwanza, namshukuru Mwenyezi mungu kwa kunijalia afya njema, ustahimilifu na uwezo wa kuikamilisha kazi hii.

Nawashukuru kwa dhati wasimamizi wangu Dkt. Jerono na Dkt. Mungania kwa kunielekeza. Mchango wenu katika kuihakiki kazi yangu hii na kujitolea kwenu kumenifaa sana. Daima nitawashukuru.

Hali kadhalika, nawashukuru wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili walionifunza kama vile Dkt. Jerono, Dkt Mungania, Prof. Iribemwangi, Prof. Rayya, Prof. Mbatia, Prof. Kineene, Dkt Sanja, Dkt Zaja, Dkt. Jefwa na Prof. Mbuthia. Maarifa niliyopata darasani kutoka kwenu yatazidi kunifaa hasa katika tasnia ya Kiswahili.

Nawashukuru pia wazazi wangu wapendwa Eric Kisoi na Prisca Yego kwa kunipa malezi bora na elimu. Mungu awape maisha marefu.

Shukrani za kipekee kwa mpenzi mume wangu Bobson Kambale Shihugwa. Umenifadhili kwa hali na mali kuhakikisha kwamba nimefaulu. Jalali akujalie baraka tumbi nzima maishani. Sitawasahau wanangu Mark, Donatta na Melissa. Asanteni kwa Subira mliyokuwa nayo kila nilipoadimika kwa sababu ya kuzamia vitabuni. Nawapenda sana na mungu awape ufanisi na maisha marefu duniani.

## IKISIRI

Utafiti huu unachanganua jinsi maneno yanavyokopwa na Kiarror kutoka lugha ya Kiswahili na kufanywa yakubalike kifonolojia na kimofolojia katika lugha ya Kiarror kwa kuzingatia muundo wa kisarufi wa lugha hiyo. Kiswahili na Kiarror huwa na mifumo tofauti ya kifonolojia na kimofolojia. Kwa mfano, utafiti huu ulibaini kuwepo kwa fonimu za Kiarror ambazo hazipo katika fonolojia ya Kiswahili, na vilevile kuwepo kwa fonimu za Kiswahili ambazo hazipo katika fonolojia ya Kiarror. Aidha, kuna tofauti baina ya miundo ya silabi pendelewa za Kiarror na silabi pendelewa za Kiswahili. Pia lugha hizi hutofautiana katika uambishaji wa maneno kiidadi. Kwa vile maneno yakopwayo sharti yazingatie masharti ya lugha kopaji ili yaweze kukubalika katika mfumo wa lugha kopaji, maneno yanapokopwa na Kiarror kutoka Kiswahili, hupitia michakato anuwai ya kifonolojia na ya kimofolojia ili yawe na miundo inayokubaliana na mfumo wa kimofofonolojia wa lahaja ya Kiarror. Licha ya utafiti huu kuchanganua michakato hiyo, ulilenga pia kubainisha sababu za michakato hiyo na athari zake katika maneno mkopo. Nadharia ambayo iliongoza utafiti huu ni nadharia ya fonolojia zalishi Asilia. Nadharia hii imetumika ili kueleza michakato ya kimofofonemiki inayohusika katika ukopaji na utohozi wa maneno mkopo ya lugha ya Kiarror kutoka lugha ya Kiswahili.

## FASILI YA ISTILAHI

**Lugha kopeshi-** Ni lugha ambayo maneno yanaazimwa au kuingizwa katika lugha nyingine. Kwa mujibu wa utafiti huu, ni lugha ya Kiswahili.

**Lugha kopaji-** Ni lugha ambayo inaazima maneno kutoka kwa lugha nyingine. Kwa mujibu wa utafiti huu, ni lahaja ya Kiarror.

## ORODHA YA ISHARA NA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| [ ] | Uwakilishi wa kifonetiki |
| / / | Uwakilishi wa fonimu |
| → | Inabadilika kuwa |
| / | Katika mazingira ya |
| $ | mpaka wa silabi |
| # | mpaka wa neno |
| I | Irabu |
| K | Konsonanti |
| FZ | Fonolojia Zalishi |
| FZA | Fonolojia Zalishi Asilia |
| Kps | sifa ya kipasuo |
| Naz | sifa ya unazali |
| Mid-meno | sifa ya mdomo-meno |
| Kkg | sifa ya kaakaa gumu |
| Kkl | sifa ya kaakaa laini |
| Krz | sifa ya kikwaruzo |
| Msi | umbo la msingi |
| Upi | umbo la upili |
| Umj | umoja |
| Wgi | wingi |

**YAFUATAYO**

TABARUKU ........ iii
SHUKRANI ........ iv
IKISIRI ........ v
FASILI YA ISTILAHI ........ vi
ORODHA YA ISHARA NA VIFUPISHO ........ vii
YAFUATAYO ........ viii
SURA YA KWANZA ........ 1
1.1 Usuli wa mada ........ 1
1.2 Tatizo la utafiti ........ 3
1.3 Maswali ya utafiti ........ 4
1.4 Malengo ya utafiti ........ 4
1.5 Sababu za kuteua mada ........ 5
1.6 Upeo na Mipaka ya utafiti ........ 6
1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada ........ 6
1.8.1 Maandishi ya kijumla kuhusu nadharia ........ 6
1.8.2 Maandishi ya Kijumla Kuhusu Lugha ya Kitugen ........ 8
1.8.3 Yaliyoandikwa Kuhusu ukopaji na utohozi ........ 9
1.9 Msingi wa kinadharia ........ 13
1.9.1 Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ........ 13
1.9.2 Masharti ya kimsingi katika Fonolojia Zalishi Asilia ........ 14
1.9.3 Kanuni za Fonolojia Zalishi Asilia ........ 16
1.10 Mbinu za utafiti ........ 18

1.10.1 Uteuzi wa sampuli ........ 19
1.10.2 Ukusanyaji data ........ 19
1.10.3 Uchanganuzi wa data ........ 20
1.10.4 Uwasilishaji wa data ........ 20
1.11 Hitimisho ........ 21
SURA YA PILI ........ 22
FONOLOJIA YA KIARROR ........ 22
2.1 Utangulizi ........ 22
2.2 Fonimu za Kiarror ........ 22
2.2.1 Irabu za Kiarror ........ 22
2.2.2 Konsonanti za Kiarror ........ 29
2.3 Fonimu za kiswahili ........ 35
2.3 Muundo wa silabi katika Kiarror ........ 36
2.3.1 Silabi wazi ........ 36
2.3.2 Silabi funge ........ 39
2.4 Silabi za Kiswahili ........ 41
2.5 Hitimisho ........ 41
SURA YA TATU ........ 42
UTOHOZI KIFONOLOJIA WA MANENO MKOPO YA KIARROR KUTOKA KISWAHILI ........ 42
3.1 Utangulizi ........ 42
3.2 Utohozi wa irabu ........ 42
3.2.1 Udondoshaji wa irabu ........ 43
3.2.2 Uchopekaji wa irabu ........ 45

3.2.3 Uyeyushaji ........................................................................................................ 46
3.2.4 Uwiano wa irabu ................................................................................................ 47
3.2.5 Urefushaji wa irabu ............................................................................................ 48
3.3 Utohozi wa konsonanti ........................................................................................... 48
3.3.1 Kuimarika na kudhoofika kwa konsonanti ............................................................. 49
3.3.2 Uchopekaji wa konsonanti ................................................................................... 56
3.3.3 Udondoshaji wa konsonanti ................................................................................. 57
3.3.4 Ubadala wa konsonanti ....................................................................................... 59
3.4 Utohozi wa silabi .................................................................................................... 60
3.4.1 Udondoshaji wa silabi .......................................................................................... 61
3.4.2 Uchopekaji wa silabi ............................................................................................ 61
3.5 Hitimisho ................................................................................................................ 63
SURA YA NNE .............................................................................................................. 64
UTOHOZI KIMOFOLOJIA WA MANENO MKOPO YA KIARROR KUTOKA KISWAHILI ........................................................................................................................ 64
4.0 Utangulizi ................................................................................................................ 64
4.1 Mofolojia ya nomino za Kiswahili ............................................................................ 64
4.2 Uainishaji wa nomino za Kiarror ............................................................................. 65
4.2.1 Nomino za Kiarror katika umbo la msingi ............................................................. 65
4.2.2 Utohozi kimofolojia wa nomino mkopo katika umbo la msingi ................................ 70
4.3 Nomino za upili ......................................................................................................... 72
4.3.1 Nomino zinazochukua viambishi vya umoja ........................................................... 72
4.3.2 Nomino zinazoambishwa wingi ............................................................................... 73
4.3.3 Nomino zinazoambishwa umoja na wingi ............................................................... 74

4.3.4 Nomino zisizoambishwa umoja wala wingi ..... 74
4.3.5 Uambishaji wa nomino mkopo katika umbo la upili ..... 75
4.4 Mifanyiko ya kimofolojia ya utohozi wa nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili..... 76
4.6 Hitimisho..... 78
SURA YA TANO ..... 79
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..... 79
5.0 Utangulizi..... 79
5.1 Mukhtasari wa matokeo ..... 79
5.2 Hitimisho..... 80
5.3 Mapendekezo ..... 81
MAREJELEO ..... 82
KIAMBATISHO..... 84
MANENO MKOPO YA KIARROR KUTOKA KISWAHILI ..... 84

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Usuli wa mada

Ukopaji ni tokeo la mtagusano baina ya lugha moja na nyingine na huwa mojawapo wa mbinu zinazotumiwa na lugha mbalimbali kujitajirisha na kujikuza kimsamiati (Odlin, 1989). El-Khafaifi (1985) anaeleza kuwa lugha yoyote kwa wakati wowote huweza kukumbwa na hitaji la kukopa ili kukidhi mahitaji yake ya kimawasiliano. Hata hivyo, lugha mbalimbali hutofautiana kutokana na vipengele vya kileksika vinavyokopa. Aidha, michakato ya utohozi wa maneno mkopo katika lugha mbalimbali hutegemea tofauti zao za kimuundo kati ya lugha kopaji na lugha kopeshi.

Utafiti huu unahusu uchanganuzi wa kimofofonolojia wa maneno mkopo yanayokopwa na Kiarror kutoka kiswahili. Kiarror ni lahaja ya Kitugen inayozungumzwa na jamii ya watu waitwao Waarror, wanaoishi katika kaunti ya Baringo, Kenya. Tofauti na Kiarror ambacho ni Kinailoti, Kiswahili ni lugha ya Kibantu. Wengi wa Waswahili hupatikana katika pwani ya Afrika Mashariki (Mwita 2009). Mbaabu (1991) anaeleza kuwa hata kabla ya majilio ya wamishenari na wakoloni, lugha ya Kiswahili ilikuwa tayari imeenea katika sehemu nyingi za bara nchini Kenya kwa njia ya biashara. Misafara ya wafanyabiashara wa masafa marefu kutoka pwani aghalabu walitumia Kiswahili kuendesha shughuli zao za uuzaji, ununuzi na ubadilishanaji wa bidhaa, basi ikawa sharti wafanyibiashara wa bara wajifunze angalau misamiati michache sahili ya Kiswahili.

Ueneaji wa lugha ya Kiswahili ulikithiri hasa baada ya kuja kwa wakoloni na wamishenari ambao walikuwa wakitumia lugha ya Kiswahili kuendesha shughuli zao hasa zilizowahusisha Waafrika. Baada ya kuondoka kwa wakoloni, sera ya serikali ya Kenya ilikipa Kiswahili hadhi ya juu kuliko lugha nyinginezo za kiasili kwa kuifanya lugha ya taifa. Aidha, Kiswahili kikawa kinafunzwa katika shule za msingi na za upili na katika vyuo mbalimbali. Lugha hii inatumika sana katika kuendesha shughuli za kitaifa, shughuli za kidini na za kibiashara. Kiswahili pia hutumika katika kutangazia kwenye vyombo mbalimbali vya habari. Hivyo basi Kiswahili kimekuwa lingua-franka Afrika Mashariki ambapo mamilioni ya watu, wakiwemo Waarror, wanaitumia kama lugha yao ya pili.

Baadhi ya maneno yanayotumika katika shughuli za kawaida miongoni mwa Waarror yana asili ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu Kiarror kimetagusana na Kiswahili kwa muda mrefu uliosababisha Kiarror kukopa pakubwa kutoka Kiswahili katika kujaribu kurutubisha msamiati

wake. Robins (1980) anaeleza kuwa kila kukiwa na mitagusano ya aina yoyote ya kitamaduni baina ya wazungumzaji wa lugha mbili tofauti, wazungumzaji wa mojawapo wa lugha zinazotagusana huweza kutumia maneno kutoka lugha inayotagusana nayo kutaja vitu, michakato, tabia, mpangilio au hata mawazo ambayo maneno ya kuyarejelea hayapatikani katika lugha yao. Hii ni sababu mojawapo inayoifanya lahaja ya Kiarror kukopa kutoka Kiswahili hasa misamiati inayorejelea elimu ya kimagharibi, dini za kikristo na kiislamu na teknolojia. Mambo haya mageni yameingizwa katika utamaduni wa Kiarror kutokana na mitagusano yake ya muda mrefu na lugha ya Kiswahili.

Langacker (1967) anadai kuwa kwa kiwango kikubwa, maneno yakopwayo katika lugha ni yale ambayo yanarejelea vitu na dhana zisizo za asili ya lugha inayokopa kwa vile wasemaji wa lugha huona kuwa ni rahisi kukopa neno linalorejelea dhana fulani kuliko kuunda neno jipya ili kurejelea dhana hiyo. Aidha, Gray (1964) anataja sababu mbili kuu zinazoifanya lugha kukopa kutoka kwa nyingine. Kwanza, anaeleza kuwa neno hukopwa kwa kuwa linasimamia kitu au dhana ambayo haikuwa imejulikana katika jamii lugha inayokopa. Kwa mfano, kabla ya kupokea elimu ya kimagharibi, Waarror hawakuwa na dhana inayowakilisha vitu kama vile kitabu, kalamu na gari. Hivyo basi, kuja kwa elimu kulileta mtagusano baina ya lugha ya Kiarror na Kiswahili uliosababisha Kiarror kukopa misamiati hiyo na kuitohoa ili ifuate mfumo wa Kiarror, mathalan:

| | Kiarror | Kiswahili |
|---|---|---|
| | **Kiarror** | **Kiswahili** |
| (1) | Kilamet | kalamu |

Aidha, Gray (1964) anaendelea kueleza kuwa lugha hukopa kwa kusukumwa na kasumba ya wazungumzaji wake. Anasema istilahi haikopwi tu kwa kuwa haipo katika lugha husika, bali ni kwa sababu wazungumzaji wake huionea fahari lugha yenye misamiati inayokopwa. Kwa hivyo wanakopa ili msamiati wao uonekane kuwa ndio bora zaidi. Wasemaji wa Kiarror wakati mwingine hukopa msamiati kutoka Kiswahili kwa sababu ya kasumba kuwa anayetumia msamiati mkopo ana hadhi ya juu zaidi kuliko anayetumia msamiati asilia, kwa mfano, neno la Kiswahili '**safari**' limekopwa na kutoholewa na baadhi ya Waarror likawa '**sapari**' ili litumike badala ya neno asilia **[pa:n].**

Kwa upande mwingine, kuna ukopaji unaonuiwa kurahisisha mawasiliano katika lugha inayokopa. Kuna dhana ambazo zinaweza kuhusisha matumizi ya maneno mengi katika kuzitaja ila katika

lugha kopeshi zinaweza kutajwa tu kwa neno moja. Hali hii inadhihirika wazi kupitia tarakimu za Kiarror. Lahaja ya Kiarror ina misamiati ya kurejelea baadhi ya tarakimu lakini imekopa ile ya Kiswahili ili kurahisisha mawasiliano, kwa mfano:

| | Kiswahili | msamiati mkopo | Kiarror asilia |
|---|---|---|---|
| (2) | /sabini/ | /sapini/ | /tɔmɔnwɔgik tesɔp/ |

Ukopaji wa neno huenda sambamba na urekebishaji wa neno husika ili lifuate kanuni za kifonolojia na kimofolojia za lugha au lahaja pokezi. Obuchi na Mukhwana (2009) wanaeleza kuwa lugha hukopa dhana ngeni pamoja na neno linalorejelea dhana hiyo lakini haiwezi kukopa kanuni za mfumo wa kifonolojia na kimofolojia. Kwa mantiki hii, maneno yakopwayo na Kiarror kutoka Kiswahili hufanyiwa marekebisho ili yaweze kukubalika katika mfumo wa kifonolojia na wa kimofolojia wa Kiarror ikitiliwa maanani kuwa mfumo wa kimofofonolojia wa Kiarror na wa Kiswahili huwa tofauti.

Tofauti za kifonolojia baina ya Kiarror na Kiswahili hubainika katika fonimu na silabi ambapo baadhi ya fonimu za Kiswahili hazipatikani katika fonolojia ya Kiarror, na baadhi ya miundo ya silabi za Kiarror haziko katika mfumo wa silabi za Kiswahili. Aidha, tofauti za kimofolojia, ambazo zitaangaziwa katika utafiti huu ni zile zinazotokana na uambishaji wa nomino. Kwa mfano, uambishaji kiidadi katika Kiswahili hutokea mbeleni mwa nomino ila katika kiarror uambishaji kiidadi hutokea mwishoni mwa nomino. Tofauti hizo za kimofolojia husababisha kurekebishwa kwa neno mkopo. Nadharia faafu zaidi katika kuelekeza uchanganuzi wa mabadiliko haya ni nadharia ya fonolojia zalishi asilia. Nadharia hii itatufaa katika kubaini michakato ya kimofofonolojia ambayo maneno mkopo hupitia, kisha kuelezea kanuni zinazodhibiti michakato hiyo.

### 1.2 Tatizo la utafiti

Kiswahili na Kiarror huwa na mifumo tofauti ya kifonolojia na kimofolojia kama vile, kuwepo kwa fonimu katika Kiarror ambazo hazipo katika fonolojia ya Kiswahili, na vilevile kuwepo kwa fonimu katika Kiswahili ambazo hazipo katika fonolojia ya Kiarror. Aidha, kuna tofauti baina ya miundo ya silabi pendwa za Kiarror na silabi pendwa za Kiswahili. Pia lugha hizi hutofautiana katika uambishaji wa maneno kiidadi. Kwa vile maneno yakopwayo sharti yazingatie masharti ya lugha kopaji ili yaweze kukubalika katika mfumo wa lugha kopaji, maneno yanapokopwa na

Kiarror kutoka Kiswahili, hupitia michakato anuwai ya kifonolojia na ya kimofolojia ili yawe na miundo inayokubaliana na mfumo wa kimofofonolojia wa lahaja ya Kiarror. Uchunguzi uliofanywa awali na mtafiti ulibainisha kuwa, uchanganuzi wa kimofofonolojia wa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili na kanuni zinazoongoza michakato ya kimofofonolojia ya utohozi wa maneno hayo hazijawekwa bayana na kufafanuliwa kitaaluma. Utafiti huu unajaza pengo hili la kiisimu kwa kuchunguza na kufafanua michakato ya kimofofonolojia ya maneno mkopo ya lahaja ya Kiarror yenye asili ya lugha ya Kiswahili kwa kuyaweka bayana na kueleza kanuni zinazoongoza michakato hiyo. Licha ya utafiti huu kuchanganua michakato hiyo, ulilenga pia kubainisha sababu za michakato hiyo na athari zake katika maneno mkopo.

## 1.3 Maswali ya utafiti

Maswali yafuatayo ndiyo yatakayoongoza utafiti huu:

(i) Je, maneno mkopo kutoka Kiswahili hupitia michakato gani ya kifonolojia na kimofolojia ili yaweze kukubalika katika mfumo wa kimofofonolojia wa Kiarror?

(ii) Je, ni sababu gani za kiisimu ndizo ambazo husababisha michakato mbalimbali mahususi ya utohozi wa kimofofonolojia wa maneno mkopo ya Kiarror kutoka kiswahili?

(iii) Je, ni zipi athari za utohozi wa kimofofonolojia wa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili?

## 1.4 Malengo ya utafiti

Utafiti wetu utaongozwa na malengo yafuatayo:

(i) Kuchanganua michakato ya kifonolojia na ya kimofolojia ambayo maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili hupitia ili yaweze kukubalika katika mfumo wa kimofofonolojia wa Kiarror.

(ii) Kubainisha sababu za kiisimu za michakato mbalimbali ya utohozi wa kimofofonolojia wa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili.

(iii) Kuchanganua athari za utohozi wa kimofofonolojia wa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili.

### 1.5 Sababu za kuteua mada

Ukopaji wa maneno umejitokeza kwa wingi katika Kiarror. Yapo maneno mengi ya Kiarror yaliyokopwa kutoka Kiswahili ingawa yanatamkwa kama maneno asilia ya Kiarror. Ingawa ni wazi kuwa mtu yeyote anayeelewa lugha ya Kiswahili pamoja na ile ya Kiarror anaweza kubainisha maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili, ni muhimu kulishughulikia suala hili kitaaluma. Utafiti huu unachanganua mofofonolojia ya maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili sanifu kwa madhumuni ya kuonyesha sababu za mabadiliko mbalimbali ya kifonolojia na kimofolojia na athari za kimofofonolojia ambazo maneno hayo hupata yanapokopwa. Hii ndiyo sababu mojawapo ya kuufanya utafiti huu kwa kutumia nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ili kueleza jinsi mfumo wa kimofolojia wa Kiarror husababisha michakato ya kifonolojia inayohusishwa katika utohozi wa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili na kanuni zinazoongoza michakato hiyo.

Lugha ya Kiswahili ina mfumo maalum wa kimofofonolojia na kanuni zake maalum ambazo zinastahili kuzingatiwa kila mara katika usemaji na uandishi wake. Baadhi ya wanafunzi wanaozungumza Kiarror kama lugha yao ya kwanza aghalabu hupata ugumu wa kutamka baadhi ya sauti za Kiswahili ambazo haziko katika fonolojia ya Kiarror kama vile /ð/ na /θ/. Mwalimu anayefahamu tofauti za kifonolojia baina ya Kiswahili na Kiarror huwa na uwezo wa kujua matatizo wanayopitia wanafunzi wake katika kutamka na kuandika Kiswahili. Utafiti huu utapiga jeki harakati za kurekebisha makosa ya kimatamshi na kimaandishi miongoni mwa wanafunzi hao. Aidha matokeo ya utafiti huu utawafaidi walimu hasa watakapoyarejelea ili kutabiri uwezekano wa kutokea kwa makosa hayo katika matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi. Hivyo basi, wataweza kuwasaidia wanafunzi wao kuyatatua matatizo yanayotokana na athari hizo kwa njia mwafaka.

Utafiti huu utachangia katika isimu linganishi kwa vile inahusisha lugha mbili zenye mifumo tofauti ya kimofofonolojia. Watafiti wanaotaka kuilinganisha lugha ya Kiswahili na lugha nyinginezo za Kinailoti wataweza kufaidika kutokana na matokeo ya utafiti huu kwa vile utafiti wenyewe unatoa mchango mkubwa kwa kutoa ruwaza jumuishi ya kinadharia itakayotumiwa kuchanganua michakato ya kimofofonolojia inayohusishwa katika utohozi wa maneno mkopo. Aidha, wasomi wanaotarajia kuandika kamusi ya Kiswahili-Kiarror au ya Kiarror- Kiswahili watafaidika kutokana na matokeo ya utafiti huu. Utawafaidi pia wasomi wengine wenye ari ya

kutaka kufahamu na kuyaweka wazi masuala zaidi kuhusu mofofonolojia ya maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili.

### 1.6 Upeo na Mipaka ya utafiti

Ingawa Kiarror kimekopa pakubwa kutoka lugha zingine kama vile Kiingereza, Kipokot, Kisamor, Kilembus, Kiturkana na Kikeiyo, utafiti huu utajikita katika maneno mkopo kutoka Kiswahili pekee. Hii ni kwa sababu Kiswahili ni lugha rasmi na ni lugha ya taifa nchini Kenya. Maneno mkopo hayo yatachaguliwa bila kuzingatia ikiwa ni ya Kiswahili kiasilia au yamekopwa kutoka Kiarabu, Kireno au Kiingereza.

Utafiti wetu ulijikita katika maneno ya kategoria ya nomino kwa sababu nomino ndiyo kategoria inayokopwa zaidi na lugha. Bynon (1977) akimnukuu Haugen (1950) anatambua kuwa katika lugha, ile kategoria ya maneno yanayokopwa zaidi huwa kategoria ya nomino kisha vitenzi na vivumishi. Sababu nyingine ya kuteua kategoria ya nomino ni kwamba kuhusisha kategoria zote za maneno kungepanua mipaka ya utafiti kupita kiasi. Huku kungeufanya utaratibu mzima wa utafiti kuwa changamano kupita kiasi.

Utafiti huu ulifanywa kwa msingi wa nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia. Nadharia hii ilitumika katika kufafanua mifanyiko ya kifonolojia inayohusisika katika utohozi wa maneno yanayokopwa na Kiarror kutoka Kiswahili. Tulichagua nadharia hii kwa vile ndiyo inayofaa zaidi katika kudhihirisha upekee wa kila lugha.

### 1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Sehemu hii imeangazia kazi mbalimbali zilizowahi kuandikwa kuhusiana na mada. Imegawika katika visehemu viwili; kwanza kuna yaliyoandikwa kuhusu nadharia, yaliyoandikwa kuhusu lugha ya Kitugen na hatimaye yaliyoandikwa kuhusu ukopaji.

#### 1.8.1 Maandishi ya kijumla kuhusu nadharia

Madai ya msingi ya Fonolojia Zalishi Asilia, kama anavyofafanua Hooper (1976), ni ile nadhariatete inayosema kuwa kila wakati ambapo wasemaji wa lugha wanakabiliwa na uchaguzi, wao hupendelea zaidi kutumia uchanganuzi uliokitwa katika mofofonolojia kuliko ule uliokitwa katika fonolojia pekee. Hii ina maana kuwa katika kuwasiliana, msemaji na msikilizaji hujaribu

kadri wawezavyo kuzihusisha sauti na maana ya neno. Huku ndiko kutunga majumuisho yanayodhihirika katika kinachotamkwa na kuleta uangavu wa kilichokusudiwa kusemwa. Usemaji huu unaashiria kuwa majumuisho ambayo hayadhihiriki katika utamkaji na ambayo hayaleti uangavu wa kilichokusudiwa kusemwa sio halisi.

Iribemwangi (2010) anaeleza kwamba Fonolojia Zalishi Asilia hairuhusu udhahania katika kounyesha umilisi wa msemaji wa lugha. Vilevile, anaongeza kuwa nadharia hii hutambua viwango mbalimbali vya lugha kama vile fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Hii ndiyo tofauti mojawapo baina ya Fonolojia Zalishi Asilia na Fonolojia Zalishi ambayo hutambua kiwango cha kifonolojia pekee. Fonolojia Zalishi Asilia hubainisha kiwango cha kifonolojia na kiwango cha kimofolojia kwa kutumia kanuni za kifonolojia zinazohusu michakato inayobainishwa tu kifonetiki na kanuni za kimofolojia ambazo zinahusu lugha mahususi na hufanya mabadiliko makubwa zaidi ya kimuundo katika neno lote. Kuwepo kwa kanuni za kimofolojia katika Fonolojia Zalishi Asilia husaidia katika kuuondoa udhahania kwa kuweka vikwazo katika kanuni za kifonolojia.

Massamba (2011) anafafanua nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia. Anaeleza kuhusu aina za kanuni katika nadharia ya fonolojia zalishi asilia, jinsi nadharia hii inavyotumika kuelezea vipengele vya kimofolojia, nadhariatete ya uangavu wa kisemantiki na upataji lugha. Anatoa maelezo kuhusu kanuni za kifonetiki na kanuni za kimofofonemiki. Anaeleza kuwa sheria za kifonetiki, ambazo pia hurejelewa kama michakato zinafanya kazi na haziwezi kuzuiliwa au kubanwa kwa namna yoyote ile. Kanuni hizi zinafanya kazi hata katika maneno yaliyokopwa na kutoholewa kutoka lugha ngeni na zinaingilia upataji wa lugha ya kigeni. Maneno yanayokopwa na Kiarror kutoka Kiswahili hupitia michakato mbalimbali ya kiutohozi wakati yanapoingizwa katika mfumo wa kimofofonolojia wa Kiarror. Hali hii hutokea kwa sababu ya tofauti za kimuundo kati ya Kiarror na Kiswahili.

Obuchi na Mukhwana (2015) wanafafanua baadhi ya mifanyiko ya kifonolojia mathalan kudhoofika na kuimarika kwa fonimu, kudondoshwa kwa fonimu, mabadiliko ya kimetathesia (tabdili) mabadiliko ya kihaplolojia na mvutano wa irabu. Maelezo yao yalitusaidia katika kuelewa mifanyiko ya kifonolojia inayokumba fonimu wakati wa utohozi wa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili. Aidha wanaeleza kwamba, ingawa lugha hukopa msamiati haikopi mfumo wa lugha kopeshi. Hii ndiyo maana maneno yanayokopwa hulazimika kurekebishwa ili yafuate

kanuni za kimofofonolojia za lugha kopaji. Maelezo yao hata hivyo yanatolewa kwa kuzingatia lugha ya Kiswahili. Uchunguzi huu ulishughulikia lahaja ya Kiarror, yenye mfumo tofauti wa kifonolojia ikilinganishwa na Kiswahili, na ambayo hulazimika kurekebisha msamiati ambao inakopa kutoka Kiswahili kwa kuutohoa msamiati huo.

### 1.8.2 Maandishi ya Kijumla Kuhusu Lugha ya Kitugen

Toweet (1975) anataja aina mbalimbali za nomino katika Kikipsigis. Anaeleza kuwa nomino za Kikipsigis huwa na maumbo ya aina mbili; umbo la kimsingi (nomino dhahiri) na umbo la upili (nomino zisodhahiri). Umbo la kimsingi hurejelea nomino isiyo mahususi. Kwa mfano, nomino [ŋgur] hutumiwa kurejelea nguo yoyote ambayo haijatajwa kwenye muktadha. Umbo la upili [ŋgurje:] linarejelea nguo mahususi katika muktadha halisi. Umbo la kimsingi hivyo basi, hurejelea nomino zisizofahamika kimuktadha ilhali umbo la upili hurejelea nomino zinazofahamika katika muktadha mahususi. Kiarror, sawa na Kikipsigis, kina nomino zilizo na maumbo ya kimsingi na ya upili. Uambishaji tamati hutumiwa katika nomino za Kiarror ili kubainisha nomino dhahiri na nomino zisodhahiri. Hata hivyo, uchunguzi wa Toweet (1975) haufafanui jinsi nomino mkopo zinavyoambishwa ili kudhihirisha umbo la kimsingi na umbo la upili. Uchunguzi huu ulichanganua jinsi nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili huambishwa mwishoni kimakusudi ili kubainisha udhahiri na usodhahiri wazo.

Jerono (2011) aliorodhesha konsonanti na vokali za Kitugen. Maelezo yake ni kuwa Kitugen kina konsonanti kumi na sita na irabu tisa; irabu fupi na irabu ndefu. Maelezo yake yalitufaa sana maana tuliyarejelea katika kuandika mfumo wa kifonolojia wa Kiarror. Aidha, alieleza kuwa aghalabu nomino mkopo za Kitugen hutoholewa ili zikubaliane na mfumo wa kawaida kimofolojia wa Kitugen; zinaongezewa viambishi tamati kwa kuzingatia udhahiri, idadi, umiliki na jinsia. Hata hivyo, kazi hii imetaja tu kuwa maneno mkopo aghalabu hurekebishwa ili yakubaliane na mfumo wa lugha pokezi ila haijaeleza bayana michakato ya kifonolojia na kimofolojia ambayo maneno hayo hupitia. Utafiti huu wetu ulichanganua michakato ya kiutohozi ambayo maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili hupitia ili yakubalike katika mfumo wa kimofofonolojia wa Kiarror.

Boen (2014) alichunguza nomino mkopo za Kinandi kutoka Kiingereza na Kiswahili. Alichanganua mabadiliko ya kimofofonemiki ambayo nomino hizo hupitia zinapotoholewa katika Kinandi kwa kutumia nadharia ya fonolojia zalishi asilia. Kinandi na Kiarror zina asili moja ya

Kikalenjin, hivyo basi zinakaribiana sana kimuundo. Maelezo yake kuhusu fonolojia vipandesauti ya Kinandi yalitufaa pakubwa katika kujenga fonolojia vipandesauti ya Kiarror. Hata hivyo, kazi hii yake haichanganui sababu za kiisimu na athari za mabadiliko ya kimofolojia katika utohozi wa maneno mkopo ambayo utafiti huu ulizichanganua. Kazi yake pia haijaeleza sababu za kutobadilika kimuundo kwa baadhi ya maneno mkopo ila uchunguzi huu wetu ulichanganua sababu hizo.

Kandagor na Sawe (2014) wanachunguza miundo ya silabi katika Kitugen na Kikipsigis. Wanachanganua jinsi Kitugen na Kikipsigis hugeuza miundo ya silabi za maneno yanayokopwa kutoka Kiswahili. Utohozi wa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili aghalabu unahusu ugeuzaji miundo wa silabi za maneno hayo. Aidha, wanaeleza kuwa ugeuzaji wa miundo ya silabi ni mchakato wa kimofofonolojia ambao hutumika katika uundaji wa maneno katika lugha yoyote ile. Ingawa katika uchanganuzi wao hawakuonyesha michakato ya kifonolojia inayohusishwa katika ugeuzi wa silabi za maneno yanayokopwa kutoka kiswahili, uchanganuzi wao ulitusaidia katika kueleza miundo ya silabi katika Kiarror na kuonyesha tofauti zilizopo kati ya miundo hii na miundo ya silabi za Kiswahili.

### 1.8.3 Yaliyoandikwa Kuhusu ukopaji na utohozi

Langacker (1967) anaeleza sababu za ukopaji wa leksimu na athari yake katika lugha lengwa. Anadai kuwa ni kupitia kwa ukopaji ndipo lugha mbalimbali huathiriana. Kiswahili kimesaidia katika ukuaji wa Kiarror kwa kukiongezea maneno mkopo, hasa yale maneno yanayorejelea dhana zisizokuwa katika utamaduni wa Kiarror. Kwa upande mwingine, Odlin (1989) anaeleza kwamba athari za fonolojia ya lugha ya kwanza zinaweza kudhihirika hasa katika matamshi ya mzungumzaji (mzawa wa lugha kopaji) aliye na ugumu wa kuimudu lugha kopeshi. Wazungumzaji wenye asili ya Kiarror aghalabu hujumlisha au kuhamisha kanuni za kifonolojia za Kiarror kwa Kiswahili. Kwa mfano, baadhi ya Waarror wanapozungumza au kuandika Kiswahili, hufanya makosa kama katika sentensi ifuatayo, mzungumzaji ameimarisha kikwamizo (-ghuna) cha mdomo-meno /f/ katika kusema [pundi] badala ya [fundi]. Hii ni kwa sababu konsonanti /f/ haipo katika Kiarror, kwa hivyo /f/ hubadilishwa kuwa /p/ katika mazingira ya kutangulia irabu ili kurahisisha matamshi. Aidha, katika sentensi ifuatayo, kipasuo (-ghuna) /p/ kimedhoofishwa kuwa kipasuo (ghuna) /b/ katika [mbera] kwa sababu kipasuo cha midomo

kisicho na mghuno /p/ kikifuata nazali /m/ ya midomo katika neno, Kiarror hukibadilisha kuwa /b/ ili kurahisisha utamkaji wa neno.

(3) Pundi amenunua mbira. (Fundi amenunua mpira.)

Scotton (1972) anafafanua utohozi wa maneno mkopo ya Kiteso kutoka lugha jirani za Kibantu na Kinailoti. Utafiti wake unachunguza mikakati ya kutambua maneno ya kiasili na yale yaliyokopwa. Ingawa utafiti wake haujaoanishwa na nadharia yoyote, umetumiwa kuchambua michakato ya kimofolojia, kifonolojia na ya kisemantiki iliyotumiwa kutohoa maneno hayo. Utafiti huu wake ulitusaidia katika kuchanganua michakato inayohusishwa katika kuyatohoa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili.

Lehman (1972) anaeleza kuwa maneno yanapokopwa, hupitia katika michakato fulani ili yakubaliwe na mfumo wa kisarufi wa lugha pokezi. Kwa kurejelea maneno mkopo ya Kiarror (lugha kopaji) kutoka Kiswahili (lugha kopeshi), mageuzi hufanywa ili yawe na miundo inayokubaliana na mfumo wa kimofofonolojia wa lahaja ya Kiarror. Kwa mfano, nomino za Kiswahili zikiwa katika wingi, viambishi vya idadi huambatishwa kwenye mzizi wa neno kama viambishi awali. Vinginevyo, katika lahaja ya Kiarror, viambishi vya idadi huambishwa kwenye mzizi kama viambishi tamati.

Wardhaugh (1972) anataja kuwa ukopaji ni njia mojawapo ya kuongeza msamiati mpya katika lugha. Mzungumzaji wa lugha anapokosa neno la kurejelea kitu fulani ilhali mzungumzaji wa lugha nyingine analo neno la kurejelea kitu kicho hicho, basi mzungumzaji wa lugha ya kwanza atakopa neno kutoka kwa mzungumzaji wa lugha ya pili. Kauli ya Wardhaugh inalandana vyema na hali ilivyo kwamba kuna msamiati ambao haungeweza kupatikana katika Kiarror pasipo kukopwa kwao kutoka Kiswahili, mathalan neno ‘kilamet’ ambalo limekopwa kutoka kwa neno la Kiswahili ‘kalamu’.

Odlin (1989) anafafanua aina mbili za ukopaji; ukopaji kiutamaduni na ukopaji msingi. Ukopaji kiutamaduni unarejelea ukopaji wa msamiati wa dhana ngeni katika lugha kopaji. Msamiati unaorejelea elimu ya kimagharibi, usafiri wa kutumia mbinu za kimakanika aidha barabarani, majini, au angani, vyakula vya kigeni, dini na hali ngeni za kimaisha umeingizwa kwa Kiarror kwa njia hii. Kwa upande mwingine, ukopaji msingi ni ukopaji wa msamiati unaorejelea dhana zilizo na msamiati asilia. Maneno yanayokopwa kwa njia hii huweza kutumiwa na wasemaji wa lugha

kopaji badala ya maneno asilia. Matumizi ya muda mrefu ya maneno haya ya mkopo huweza kuyafanya yachukue nafasi ya maneno asilia, hatimaye, maneno asilia huacha kutumiwa kisha huweza kupotea.

Ingawa ukopaji kiutamaduni unatajirisha lahaja ya Kiarror kimsamiati, ukopaji msingi umeiweka lahaja hii katika hatari ya kuyapoteza matumizi ya baadhi ya maneno yake asilia. Odlin (1989) anataja mfano wa Kidyirbal cha kizazi kipya kama kinavyozungumzwa na wazawa asilia wa kaskazini mwa Australia. Anaeleza kuwa ukopaji kiutamaduni umeathiri Kidyirbal kiasi kwamba matumizi yake yamekuwa yakififia polepole kwa muda kama tokeo la wazungumzaji wake hasa vijana na watoto kupendelea Kiingereza. Anaeleza kuwa wazungumzaji hao aghalabu hawafahamu maneno yanayorejelea desturi zao kama vile upishi, kwa hivyo mara nyingi wao hutumia maneno ya Kiingereza. Ingawa ukopaji huweza kuathiri lugha kisemantiki, kama vile kusababisha upanuzi wa maana ya leksimu, ukopaji hauwezi kuathiri fonetiki na fonolojia ya lugha kopaji. Kwa mujibu wa Schmidt (1985), matamshi ya maneno mkopo kwa wasemaji wa lugha kopaji hulandana na matamshi ya maneno asilia ya lugha hiyo. Ingawa Kiarror kimekopa maneno kutoka Kiswahili, matamshi ya maneno hayo hutokea kama yalivyo katika maneno asilia ya Kiarror.

Kiango (1991) anaeleza kuwa marekebisho hufanywa katika istilahi za kigeni ili zilandane na mfumo wa kifonolojia wa lugha inayokopa. Maelezo ya Kiango (1991) yametuwezesha kubaini kuwa maneno ya Kiswahili yanapotoholewa katika Kiarror, maumbo yao hubadilika kwani maneno yenyewe hufanyiwa michakato ya kimofofonemiki ambayo inahakikisha kwamba maneno yenyewe yanashabihiana na yale asilia ya Kiarror. Hali hii hutokea kwa sababu lugha hizi mbili ni tofauti kimuundo. Maelezo haya yalikuwa kichocheo kwetu cha kutaka kujua ni kwa njia gani konsonanti na irabu za maneno yanayokopwa kutoka Kiswahili zinabadilika ili zioane na muundo wa kimofofonolojia wa Kiarror.

Wa Mberia (1993) anachunguza mofofonolojia ya Kitharaka kwa kutumia nadharia ya fonolojia zalishi asilia. Anachunguza michakato ya kifonolojia katika lugha hiyo na pia anafafanua kanuni zinazotawala michakato hiyo. Vilevile, anatalii mabadiliko ya fonimu za msamiati unaokopwa na Kitharaka kutoka Kiswahili. Ingawa Kitharaka ni lugha ya Kibantu, maelezo yake yalitunufaisha hasa katika kuelewa jinsi ya kutumia Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia katika kazi yetu katika

kuchunguza mabadiliko ya kimofonolojia yanayokumba maneno yanapokopwa na Kiarror kutoka Kiswahili.

Mathooko (2006) akijadili utohozi, anasema kuwa mbinu hii huwa na upungufu mkubwa hasa ikiwa utaratibu hautafuatwa. Kwa maoni yetu, ingekuwa vyema ikiwa, neno likikopwa, patakuwepo makubaliano ya mifanyiko inayohusishwa ili kupata neno linaloafikiana na mfumo wa kisarufi wa lugha kopaji. Hata hivyo, kuna maneno ambayo yanapotoholewa huunda maneno zaidi ya moja, na maneno yanayoundwa yanahusisha mifanyiko tofauti ya kifonolojia. Hali hii inabainika katika baadhi ya maneno yaliyokopwa na kutoholewa, mathalan:

| | **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|---|
| (4) | /dereva/ | /ndɛrɛpa/ |
| (5) | /dereva/ | /ndɔrɔpɔin/ |

Katika mfano (5), mchakato wa utohozi wa neno /dereva/ unahusisha unazalishaji wa konsonanti /d/ kuwa /nd/. Konsonanti nazalishi ni konsonanti ambazo huchukuliwa kama sauti moja wakati zinapotamkwa pamoja. Kipasuo ghuna cha ufizi /d/ kikitokea mwanzoni mwa neno mkopo, Kiarror huongeza nazali ya ufizi /n/ kwa sababu konsonanti /d/ haipo katika mfumo wa kifonolojia wa Kiarror. Aidha, kipasuo ghuna cha midomo /b/ huimarishwa na kuwa /p/ kwa vile fonolojia ya Kiarror haina kipasuo /b/. Katika mfano (6), neno /dereva/ limegeuzwa kuwa /ndɔrɔpɔin/ ili kudhihirisha umoja wake. Kiarror hutumia kiambishi {in} katika kudhihirisha umoja wa baadhi ya nomino, na ili kurahisisha utamkaji, irabu /ɛ/ na /a/ zinawiana na kuwa /ɔ/. Maelezo ya mifanyiko hii yatatolewa kwa kina zaidi katika sura ya tatu ya utafiti huu.

Iribemwangi (2008) anataja kuwa ukopaji huwa muhimu hasa ili lugha iende sambamba na maendeleo yanayotokea katika sehemu ambazo lugha inatumika. Utafiti wake ulinufaisha utafiti huu kwa vile mengi ya maneno mkopo yamekopwa kutokana na ukweli kuwa, kulikuwa na pengo la kisemantiki kwa dhana inayorejelewa na neno mkopo katika lugha kopaji. Aidha, ukopaji ni mchakato ambao unaendelea kadri lugha inavyoendelea kukua. Hivyo basi, ukopaji husaidia lugha kukua kwa kuiongezea misamiati hasa inayohusu vitu na dhana ngeni.

Habwe, Matei na Nyonje (2010) wanaeleza kuwa utohozi hutumika katika kufidia kukosekana kwa istilahi fulani katika utamaduni wa lugha kopaji. Istilahi husika inapokopwa, inaundwa upya kwa kuzingatia mfumo wa kifonolojia wa lugha kopaji. Kwa kufuata maelezo haya, lugha kopeshi

ni lugha ya Kiswahili nayo lugha kopaji ni Kiarror. Katika utamaduni wa Kiarror, kuna dhana ambazo hazikuwepo ila zimeletwa na elimu na teknolojia kama vile:

| | Kiswahili | Kiarror |
|---|---|---|
| (6) | /gari/ | /kari/ |

### 1.9 Msingi wa kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia. Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia (FZA) ilitumika katika kuzichanganua mifanyiko ya kifonolojia katika maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili. FZA pia ilitumika katika kuvibainisha vigezo vya kifonolojia na vya kimofolojia vinavyodhibiti utohozi wa kimofofonolojia ya maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili.

#### 1.9.1 Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia

Fonolojia Zalishi Asilia ni mtazamo wa kueleza lugha kimofofonolojia ulioasisiwa na Venneman (1972, 1974), Hooper (1975, 1976, 1979), Hudson (1975) na Rudes (1976) miongoni mwa wengine. Vennemenn (1972) aligundua kuwa kulikuwa na udhahania mwingi katika uwasilishaji wa elementi katika Fonolojia Zalishi (FZ) kama vile ubia katika fonolojia zalishi za lugha, kanuni za kifonolojia na mpango wa ishara za irabu. Mwanafunzi wake, Hooper (1976, 1979) akaifafanua zaidi kwa kuonyesha jinsi Zonolojia Zalishi Asilia ilivyo na uwezo wa kuonyesha umilisi wa mzawa wa lugha. Lengo la wananadharia hao lilikuwa ni kuivumbua nadharia iliyo na uwezo wa kueleza masuala kuhusu lugha asilia. Walitaka nadharia isiyokuwa na nguvu zaidi kiasi cha kueleza au kutabiri matukio ambayo hayapatikani katika lugha asilia.

Madai ya msingi katika Fonolojia Zalishi Asilia ni kuwa wasemaji wa lugha katika kuyatamka maneno ya lugha husika, hutunga majumuisho yanayodhihirika katika kinachotamkwa na kuleta uangavu wa kinachokusudiwa (Hooper 1976). Usemaji huu unaashiria kuwa majumuisho yasiyodhihirika katika utamkaji na yasiyoleta uangavu wa kile kilichokusudiwa kusemwa, si halisi. Hooper (1976) anadai kuwa majumuisho ambayo yanadhihirika na yanayoleta uangavu huweza kukosolewa ilhali yale yaliyo ya kidhahania katika Fonolojia Zalishi hayawezi; na kuwa kwa vile majumuisho ambayo yanadhihirika kiusemaji na yanayoleta uangavu wa wazi wazi wa kile

kilichokusudiwa ni halisi zaidi, basi yanatupa msingi madhubuti ambao kwao tunaweza kujenga kanuni madhubuti za kimajumui katika fonolojia na mofolojia.

Kwa mujibu wa Massamba (2011), nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ni mtazamo uliozuka kwa minajili ya kuyatatua baadhi ya matatizo yaliyoaminika kwamba yalitokana na upungufu wa Nadharia ya Fonolojia Zalishi (FZ). Fonolojia Zalishi ni mtazamo uliobainika katika kazi za wanaisimu kama vile Noam Chomsky na Morris Halle za mwaka wa 1968. Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia inapinga mambo ambayo yalidhaniwa na waasisi wake kuwa hayafai kama vile udhahania wake katika uwakilishaji wa vipengele vya kifonolojia na urasmi wa kanuni zake. Kwa jumla, Fonolojia Zalishi ilishikilia kwamba lugha zote zina sifa bia.

Kulingana na waasisi wake, Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia iliibuka kwa sababu ya udhaifu wa Fonolojia Zalishi ambayo ilikuwa imepewa uwezo mkubwa sana kiasi cha kukosa kuzingatia mfumo wa lugha asilia. Hivyo basi, haingeweza kuwakilisha uasilia wa lugha. Kimsingi, Fonolojia Zalishi Asilia inahusu jaribio la kurekebisha Fonolojia Zalishi kindani wala si nadharia tofauti. Kwa hivyo, ingawa Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia inapinga udhahania wa Fonolojia Zalishi, ina madai sawa na ya Fonolojia Zalishi kuhusu kanuni za kifonolojia kama vile udhoofikaji na uimarikaji wa konsonanti, uchopekaji na udondoshaji wa fonimu.

### 1.9.2 Masharti ya kimsingi katika Fonolojia Zalishi Asilia

Hooper (1976) anayataja masharti matatu ambayo yangetatua matatizo yaliyotokana na Fonolojia Zalishi kama vile udhahania. Kanuni zenyewe ni zifuatazo:

(i) Sharti la ujumlishaji sahihi
(ii) Sharti la kuimarisha uasilia
(iii) Kanuni inayozuia kulazimishwa kwa sheria

#### (i) Sharti la ujumlishaji sahihi

Sharti hili hudhibiti kanuni za kifonolojia kwa kuondoa matumizi ya uwezekano. Kudhibitiwa huku kumeifanya iweze kuchunguza lugha katika uasilia wake. Wasemaji asilia wa lugha huunda

majumuisho ya lugha yao ambayo yanadhihirika katika umbo nje ili kuuondoa udhahania. Hii ina maana kuwa umbo ndani la neno linaweza kutabirika kutokana na umbo nje na hali hii inaonyesha kuwa majumuisho yanayodhihirishwa ni asilia na huwa msingi wa uundaji wa kanuni halisi za kifonolojia na kimofolojia. Fonolojia Zalishi Asilia inatambua kuwa michakato ya lugha ni changamano na haiwezi kuainishwa kwa njia ya kuridhisha bila kuhusisha viwango mbalimbali vya lugha kama vile fonolojia, mofolojia, semantiki na sintaksia. Pia inatambua uhusiano baina ya kiwango cha fonolojia na mofolojia katika lugha yoyote ile. Kwa mfano, katika utamkaji wa maneno ya Kiingereza, kanuni hizi zinaamuru ikiwa patakuwa na mghuno au la. Mfano ni ule wa sauti ya Kiingereza **/s/** inayotumika kuonyesha wingi wa nomino. Sauti **/s/** hupata sifa za mghuno katika maneno mengine kama vile **'pigs'** na **'needles'** kwa sababu ya ujirani wake na sauti ghuna. Katika maneno mengine kama vile **'maps'** na **'pirates'** haipati mghuno kwa sababu ya ujirani wake na sauti zisizokuwa na mghuno.

(ii) **Sharti la kuimarisha uasilia**

Sharti hili linadhibiti udhahania wa maumbo ndani. Linapendekeza ya kwamba maumbo ndani yanapaswa kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na maumbo nje na yawakilishwe kifonetiki. Linadai uangavu kati ya umbo ndani na umbo nje. Uhusiano huu wa moja kwa moja kati ya umbo ndani na umbo nje huonyesha michakato inayotokea hivyo kuepuka udhahania katika sarufi. Sharti hili linasisitiza kuwa kila kanuni ya kisarufi inayopata motisha kifonolojia lazima ionyeshe ujumlishaji kuhusu muundo nje wa neno.

**(iii) Sharti linalozuia kulazimishwa kwa sheria**

Sharti hili linadhibiti jinsi sheria zinavyotumika. Linadai kuwa kanuni hazipaswi kulazimishwa katika lugha ila zinaweza kutumika tu ikiwa mfumo wa lugha husika unaweza kukubali kanuni zenyewe. Kanuni zitumike kwa utaratibu na kila kanuni iweze kujisimamia. Linadhibiti uwasilishaji mlalo wa kanuni kwa kusisitiza kuwa kila kanuni itumike tu baada ya kuhakikisha kuwa maelezo ya kimuundo yametolewa baada ya kanuni nyingine kutumiwa. Ni sharti linalosisitiza kuwa kanuni maalum kila mara ndizo zinazopaswa kutumika kabla ya kanuni za kijumla. Katika kuchunguza lugha, sharti hili linasisitiza kuwa matukio ya kifonolojia yachunguzwe kwa kuyahusisha na matukio ya kimofolojia.

### 1.9.3 Kanuni za Fonolojia Zalishi Asilia

Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ina makundi manne makuu ya kanuni:

(i) Kanuni za kifonetiki

(ii) Kanuni za kimofolojia

(iii) Kanuni za via

(iv) Kanuni za sandhi

#### 1.9.3.1 Kanuni za Kifonetiki

Kikundi hiki kinahusisha kanuni au michakato ambayo hubainishwa tu kifonetiki, yaani inayohusu sifa za kifonetiki na mipaka ya kifonetiki kama vile mpaka wa silabi. Ni kanuni zalishi na haziwezi kuzuiliwa au kubanwa. Kanuni hizi huathiri upataji wa lugha ya pili, hivyo basi zinahusika hata katika utohozi wa maneno mkopo. Aidha, kanuni za kifonetiki ni bia kwa vile hupatikana katika lugha nyingi ulimwenguni kwa vile zinasababishwa kwa misingi ya kifonetiki. Zinatumika katika kueleza mabadiliko bia ya sauti ambayo huvuka mipaka ya lugha. Mifano ya mabadiliko hayo ni udhoofikaji na uimarishaji wa vipande sauti pamoja na miundo ya silabi. Kwa mfano, neno la Kiswahili **'meza'** likitoholewa kwa Kiarror hubadilika na kuwa **'mesa'** kama ifuatavyo:

/z/ ⟶ /s/ / [irabu] _ [irabu]

Kanuni hii itatusaidia kubainisha mabadiliko ya sauti yanayotokea wakati maneno ya Kiswahili yanapoingizwa katika Kiarror.

#### 1.9.3.2 Kanuni za Kimofolojia

Tofauti na kanuni za kifonetiki, kanuni za kimofolojia si bia bali zinahusu lugha mahususi. Kanuni hizi hufanya mabadiliko makubwa zaidi ya kimuundo katika neno lote. Ni kanuni zinazohusiana na maana katika lugha husika. Kila lugha huwa nan jia yake ya kipekee ambayo hutumia kuelezea mabadiliko mbalimbali katika mazingira ya kimofolojia n ahata ya kisintaksia, kwa mfano, jinsi mofimu fulani inavyotumika kuonyesha hali ya wingi. Katika Kiswahili, idadi ya nomino hudhihirishwa kwa njia mbalimbali kutegemea ngeli, mathalan:

**(6 a) M**tu **m**refu anatembea. - **Wa**tu warefu wa**na**tembea.

Matumizi haya ya mofimu {m}, na {wa} kudhihirisha idadi hutokea kwa upekee katika Kiswahili kwani hayadhihiriki katika lugha nyingine kama vile Kiarror ambapo sentensi iyo hiyo ingefasiriwa hivi:

**(6 b) W**entei **ch**ich na kooi. – **P**entei **p**ich cha koen.

Mofimu {w}, {ʧ} na {p} imetumika kudhihirisha idadi.

Kanuni za kimofolojia pia zinaeleza sababu za kuwepo kwa alomofu anuwai katika kubainisha wingi wa baadhi ya nomino. Kwa mfano, kanuni hizi zinaweza kutumika katika maneno ya Kiarror ambapo wingi wa nomino moja huweza kubainishwa na mofimu zaidi ya moja, kwa mfano:

| | **Umoja** | | **mzizi** | **mofimu ya wingi** | **wingi** |
|---|---|---|---|---|---|
| (7 a) | Kari | (gari) | kari | {noi} | karinoi (magari) |
| (7 b) | Kari | (gari) | kari | {s} | karis (magari) |

Neno hili lina sura mbili tofauti za mofimu ya wingi, yaani alomofu {s} na {noi}. Fonolojia pekee haiwezi kueleza mabadiliko haya bali kanuni za kimofolojia zinahitajika ili kuyaeleza kwa ukamilifu.

#### 1.9.3.3 Kanuni za via

Hizi ni kanuni ambazo zinaonyesha uhusiano wa kipekee baina ya elementi za kileksika. Zinadhihirisha uhusiano wa moja kwa moja baina ya maumbo nje, bila ya kuyakokoteza kutokana na umbo ndani. Kanuni za via hutuwezesha kuonyesha uhusiano baina ya vipengele vya leksika kama vile maneno ya Kiingereza ‘go’ na ‘went’ ambayo hutofautiana kwenye muundo nje ingawa yanazalishwa kutoka kwa muundo sawa wa ndani. Kanuni za via si zalishi, hivyo basi, vipengee vichache vinavyohusishwa na kanuni hizi ni lazima vionyeshwe ili kuvibainisha. Kwa mujibu wa Hooper (1976), msemaji wa lugha huhifadhi miundo yote tofauti akilini ingawa anafahamu kuwa kuna uhusiano baina ya miundo hiyo tofauti. Katika baadhi ya nomino za Kiarror, uhusiano huu unadhihirika ifuatavyo:

| Nomino za Kiarror: | | **umoja** | **wingi** |
|---|---|---|---|
| | **(8)** | /arta/ (mbuzi - umoja) | /no/ (mbuzi - wingi) |

Ingawa maneno /arta/ na /no/ yana maumbo tofauti, msemaji wa Kiarror anafahamu kuwa yana uhusiano wa moja kwa moja na huhifadhi maumbo yote akilini ili kurejelea dhana ya umoja na wingi.

#### 1.9.3.4 Kanuni za Sandhi

Hizi ni kanuni ambazo hutokea baina ya kanuni za kifonetiki na kanuni za kimofolojia. Kanuni hizi zinazingatia mpaka wa neno na wakati mwingine mpaka wa neno huweza kulingana na mpaka wa silabi, hivyo basi kutokea kama kanuni ya kimofofonolojia. Hii ni kwa sababu mpaka huu unaweza pia kutokea kama silabi inayotanguliza neno na inayotamatisha neno. Kanuni za sandhi zitatuwezesha kupata mwanga wa jinsi mipaka ya silabi inavyodhihirishwa na Kiarror ili kufahamu mabadiliko ya kimofofonolojia ya maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili kwa kuwa baadhi ya michakato ya utohozi wa maneno hayo mkopo hukusudia kupata miundo yenye kukubalika katika silabi za maneno ya Kiarror.

Kwa kuzingatia maelezo haya ya kimsingi, tunaweza kudai kuwa Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia inatambua viwango vya lugha kama vile fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Iribemwangi (2008) anaeleza kuwa nadharia hii inaonyesha mpaka baina ya fonolojia na mofolojia; hivyo kusababisha kuwepo kwa kanuni za kifonetiki na kanuni za kimofolojia. Kutenganishwa huku husaidia katika kutambulisha mabadiliko mbalimbali ya fonolojia, na kueleza sababu za mabadiliko hayo kwa kutumia kanuni mbalimbali. Inasaidia pia kuelezea mabadiliko mbalimbali ya fonimu ambayo hayawezi kuelezwa kifonetiki tu.

Kwa ujumla, nadharia ya fonolojia zalishi asilia inadiriki kulitatua tatizo la udhahania lililojitokeza katika fonolojia zalishi. Aidha, inatambua kiwango cha kimofolojia ambacho kilipuuzwa na nadharia ya fonolojia zalishi. Fonolojia Zalishi Asilia inatambua mabadiliko katika lugha za asili Kwa mantiki hii, nadharia hii ndiyo bora zaidi katika kueleza mabadiliko yanayotokana na ukopaji wa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili.

## 1.10 Mbinu za utafiti

Sehemu hii inaangazia jinsi sampuli ilivyoteuliwa, jinsi data zilivyokusanywa, jinsi data zilivyochanganuliwa na jinsi zilivyowasilishwa. Ukusanyaji wa data unahusu michakato yote iliyotumiwa na mtafiti ili aweze kupata nomino za Kiarror ambazo zilikopwa kutoka Kiswahili.

Katika sehemu ya uchanganuzi wa data, mtafiti alieleza mbinu alizotumia kuzikabili nomino mkopo kwa madhumuni ya kuyatimiza malengo ya utafiti.

### 1.10.1 Uteuzi wa sampuli

Sampuli ya utafiti iliteuliwa kimakusudi ili kuhakikisha kwamba data iliyokusanywa ilituwezesha kuangazia tatizo la utafiti kikamilifu. Data ya utafiti ilikusanywa katika eneo la Kipsaraman, kaunti ndogo ya Baringo Kaskazini. Mtafiti alichagua eneo hili kwa sababu ni mzawa wa Kipsaraman na wengi wa wakazi wa eneo hili aghalabu hutumia lahaja ya Kiarror kwa mawasiliano yao ya kila siku. Aidha, ana uhusiano wa karibu na baadhi ya wakazi wa eneo hilo, kwa hivyo kuna mlahaka mwema baina ya mtafiti na wengi wa wenyeji. Data katika sehemu hii ilijumuisha maneno ya Kiswahili ambayo yameweza kuingizwa kwenye mfumo wa Kiarror na ilikusanywa katika sehemu tatu: Katika kanisa la Full Gospel Kipsaraman, katika soko la Kipsaraman na katika mikutano ya kisiasa eneo la Kipsaraman.

### 1.10.2 Ukusanyaji data

Mtafiti alitumia uchunguzi wa kushiriki katika kukusanya data kanisani, sokoni na kwenye mikutano ya kisiasa. Kanisani, mtafiti alijiunga na waumini wengine kwenye ibada huku akiyanukuu mahubiri kisha baadaye kuyapitia na kuzidondoa nomino mkopo jinsi zinavyotumiwa katika mahubiri. Data iliyokusanywa kanisani ni ya maneno mkopo ya kidini. Mtafiti pia aliweza kwenda katika soko la Kipsaraman pauzwapo bidhaa mbalimbali na kuyasikiliza na kurekodi mazungumzo kwa kutumia kinasa sauti kisha baadaye akayatumia katika uchanganuzi. Alitumia kinasa sauti ambacho kilinasa mazungumzo mbalimbali kisha baadaye akayasikiliza mazungumzo hayo na kuyadondoa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili kwa kutumia ujuzi wake wa lahaja hii. Mtafiti aliweza kukusanya jumla ya maneno mkopo hamsini kutoka kila sehemu.

Utafiti uliendeshwa kwa kuzingatia maadili ya utafiti kama yanavyohitajika. Kwanza, mtafiti alihakikisha ana barua rasmi kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi pamoja na cheti cha idhini ya kufanya utafiti kutoka Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (NACOSTI). Aidha, alipata ruhusa ya kwenda nyanjani kutoka kwa wasimamizi wake. Mtafiti pia alihakikisha kuwa amezungumza na wahubiri na wasimamizi wa kanisa la Full Gospel, Kipsaraman ili kupata idhini

ya kunasa video ya mahubiri kanisani. Kanda za video zilizonaswa zilichukuliwa kwa heshima na waliohusika kuelezwa sababu za kuchukuliwa video hizo.

Maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili yaliteuliwa bila ya kuzingatia ikiwa maneno yenyewe ni ya asili ya Kiswahili au yamekopwa na Kiswahili kutoka Kiingereza, Kiarabu, Kijerumani au Kireno. Kwa kutumia umilisi wake wa lugha zote mbili, mtafiti aliweza kutambua maneno ya Kiarror yaliyokopwa kutoka Kiswahili.

### 1.10.3 Uchanganuzi wa data

Hatua ya kwanza ya uchanganuzi wa data ilihusisha kuyasikiliza mazungumzo yaliyonaswa kwa makini ili kuyadondoa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili. Data iliyonaswa katika kanda za kunasia sauti zilisikilizwa na kisha kunukuliwa katika maandishi.

Tulikuwa na jedwali lenye sehemu nne za kunakili nomino katika lugha ya Kiswahili, na nomino mkopo za Kiarror katika umoja na wingi kiothografia na kifonetiki. Maneno hayo yalinukuliwa kifonetiki kisha yakalinganishwa na maneno asilia ya Kiswahili ili kudhihirisha mabadiliko ya sauti yanayotokea wakati maneno ya Kiswahili yanapokopwa na kutoholewa kwa Kiarror. Sauti ziliainishwa ili kubainisha zile zinazobadilika. Michakato mbali mbali ya kifonolojia inayohusika katika utohozi ilitambulishwa halafu vigezo na kanuni za kimofofonolojia zilizohusika katika utohozi zikawekwa wazi. Kanuni za nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia zilitumika katika kudhibitisha mabadiliko ya kimofofonolojia yanayojiri katika utohozi wa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili. Kanuni zilizotumiwa kufafanua michakato ya kimofofonolojia ya nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili zilielezwa na kudhihirishwa. Maelezo hayo yalifafanua michakato ya kimofofonolojia inayoathiri utohozi wa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili kama vile udhoofikaji wa konsonanti, uimarikaji, uchopekaji na udondoshaji wa konsonanti na irabu. Aidha, sababu za kila mchakato zilielezwa na athari zake kuonyeshwa.

### 1.10.4 Uwasilishaji wa data

Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa kutumia maelezo, mifano, vielelezo na jedwali. Fonimu na silabi zinazobadilika zilibainishwa wazi huku michakato inayohusika katika utohozi wa fonimu na silabi husika ikitambulishwa. Aidha, utohozi wa kimofolojia wa nomino zinazokopwa na Kiarror kutoka Kiswahili ulifafanuliwa kwa kutoa mifano na maelezo ya kudhihirisha jinsi maneno ya

Kiswahili yanavyoingizwa katika mfumo wa kimofolojia wa Kiarror. Jedwali lenye sehemu nne lilitumiwa kuorodhesha maneno mkopo Kiarror kutoka Kiswahili ili kudhihirisha mabadiliko yanayotokea katika mchakato wa ukopaji na utohozi. Kwenye sehemu ya kwanza ya jedwali, maneno yaliandikwa katika Kiswahili. Sehemu ya pili na ya tatu zitakuwa na maneno mkopo yaliyo katika sehemu ya kwanza katika Kiarror, kisha unakili wa kifonetiki wa maneno hayo utaonyeshwa katika sehemu ya nne ya jedwali.

## 1.11 Hitimisho

Sura hii imefafanua masuala ya kimsingi katika uchunguzi wa kimofofonolojia wa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili. Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ndiyo iliyotumiwa kuchanganua mabadiliko ya kimofofonolojia katika utohozi maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili. Katika sehemu zinazofuata, tutadhihirisha fonolojia na mofolojia za lugha ya kiswahili na lahaja ya Kiarror. Hali hii ilifanikisha uelewa wa namna vipande sauti pamoja na maneno huingia katika utaratibu wa Kiarror kutoka Kiswahili katika utaratibu wa utohozi wa maneno mkopo.

## SURA YA PILI

## FONOLOJIA YA KIARROR

### 2.1 Utangulizi

Katika sura ya kwanza, tulionyesha kuwa Kiarror kimetagusana na Kiswahili kwa muda mrefu, hivyo kusababisha Kiarror kukopa kutoka Kiswahili. Aidha, tulieleza kuwa mfumo wa kimofofonolojia wa Kiarror huwa tofauti na ule wa Kiswahili, kwa hivyo maneno yanayokopwa kutoka Kiswahili huhitaji kufanyiwa marekebisho ili kuyawezesha kufuata kanuni za kifonolojia na za kimofolojia za Kiarror. Katika sura hii, tulijadili vipengele vya kimsingi vya kifonolojia katika Kiarror na kuvilinganisha na vya Kiswahili. Lengo la kujadili vipengele hivi lilikuwa ni kuunda misingi ambayo ingetupa mwelekeo ufaao wakati wa kushughulikia michakato ya kiutohozi inayohusishwa katika utaratibu wa ukopaji wa maneno ya Kiswahili katika Kiarror. Vipengele vya kifonolojia vilivyoshughulikiwa katika sura hii ni fonimu na silabi. Tulijadili fonimu za Kiarror na Kiswahili tukiziainisha na kueleza sifa bainifu za kila fonimu. Aidha miundo ya silabi katika Kiarror na Kiswahili ilijadiliwa. Kwa vile silabi huchukua nafasi ya kipekee katika michakato ya kifonolojia, ilikuwa ni muhimu kuonyesha tofauti za kimuundo zinazodhihirika katika silabi za Kiarror na Kiswahili ili tuweze kuelewa jinsi muundo wa silabi unavyoweza kuathiri michakato mbalimbali ya kifonolojia.

### 2.2 Fonimu za Kiarror

Fonimu za Kiarror zimeainishwa katika aina mbili; konsonanti na irabu. Kigezo cha kuzuiliwa kwa hewa wakati wa kuzitamka fonimu ndicho kilichotumika katika uainishaji huu. Irabu hutamkwa kwa kuuachilia mkondo hewa mpana ilhali konsonanti hutamkwa kwa kuuzuilia.

#### 2.2.1 Irabu za Kiarror

Kiarror kina irabu tisa za aina mbili; irabu za wakaa fupi na irabu za wakaa ndefu. Irabu za wakaa fupi ni: /a/, /e/, /i/, /o/, /u/, /I/, /ɔ/, /ɛ/, na /ʊ/. Irabu za wakaa ndefu ni: /a:/, /e:/, /i:/, /o:/, /u:/, /I:/, /ɔ:/, /ɛ:/, na /ʊ:/. Katika Kiarror, wakaa wa irabu ni sifa bainifu ambayo inaweza kubainisha maana katika maneno kama vile katika maneno '/ʧam/' na /ʧa:m/. Neno '/ʧam/' lina maana ya 'penda'

ilhali ‘/ʧa:m/’lina maana ya ‘nong’ona’. Jedwali lifuatalo linaonyesha uwakilishi wa kifonetiki na wa kiothografia wa irabu za Kiarror na jinsi zinavyotokea katika maneno.

**Kielelezo 2.4 Jedwali la irabu za Kiarror**

| **IRABU** | **OTHOGRAFIA** | **UWAKILISHI WA KIFONETIKI** | **MAANA** |
|---|---|---|---|
| I | i | [pis]<br>[kerti]<br>[ip] | Juta<br>Msitu<br>Peleka |
| i: | ii | [pi:ʧ]<br>[i:t] | Watu<br>Sikio |
| I | i | [It]<br>[sIr] | Fika<br>Andika |
| I: | ii | [rI:l]<br>[I:m] | -eupe<br>Fadhaisha |
| E | e | [tep]<br>[let] | Kaa<br>Nyuma |
| e: | ee | [pe:t]<br>[e:i] | Mchana<br>Mkono |
| ε | e | [kεt]<br>[pa:ndε]<br>[εp] | Teka<br>Mahindi<br>Kata kwa panga |

| | | | |
|---|---|---|---|
| ɛ: | ee | [pɛ:l]<br>[ɛ:i] | Choma<br>Mtamba |
| A | a | [ʧam]<br>[am]<br>[lakwa] | Penda<br>[kula]<br>Mtoto |
| a: | aa | [pa:n]<br>[sa:n] | Safari<br>Mashemeji |
| U | u | [ʧut]<br>[ut]<br>[ru] | Ingia<br>Piga risasi<br>Lala |
| u: | uu | [iʧu:t]<br>[u:i] | Vuta<br>Hama |
| ʊ | u | [ipʊt]<br>[ʊɲ] | Anguka<br>Ficha |
| ʊ: | uu | [tʊ:i]<br>[ʊ:ʧ] | -eusi<br>Umiza |
| o | o | [kolɣol]<br>[oti]<br>[porjo] | Kwapa<br>Hapa<br>Kibanda |
| o: | oo | [po:n]<br>[o:ntir] | Wachawi<br>Jipu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | [loː] | Mbali |
| ɔ | o | [kɔlɣɔl]<br>[muɣɔ]<br>[ʧeptɔ] | Ghali<br>Kibuyu<br>Msichana |
| ɔː | oo | [ʧɔːɲ]<br>[ɔːwei]<br>[uːnɔː] | Mnyama<br>Ndio<br>Ndivyo |

Katika jedwali hili, ni wazi kuwa irabu za Kiarror huweza kutokea kwenye sehemu yoyote ya neno. Zinaweza kutokea mwanzoni mwa neno kama katika maneno haya: [ɔti], [iit] na [ipʊt]. Irabu za Kiarror pia zinaweza kutokea katikati mwa neno, kwa mfano, [kɛt], [kɔlkɔl] na [ʧɔːɲ]. Kuna wakati ambapo irabu za Kiarror zinatokea mwishoni mwa neno kama inavyobainika katika maneno haya: [pai], [tʊːi] na [kɔ]. Hata hivyo, Kiarror kimeainishwa kama lugha yenye muundo wa KIK (Konsonanti-Irabu-Konsonanti) kwa vile maneno ya Kiarror kwa kiasi kikubwa huanza kwa konsonanti na kumalizikia irabu.

#### 2.2.1.1 Sifa bainifu za irabu za Kiarror

[a]

+irabu
+kati
+chini
-mviringo

[aː]

+irabu
+kati
+chini
-mviringo
+urefu

[ɛ]

+irabu
+mbele
+kati-chini
-mviringo

[ɛ]

+irabu
+mbele
+kati-chini
-mviringo
+urefu

| [o] | [o:] | [ɔ] | [ɔ:] |
|---|---|---|---|
| +irabu | +irabu | +irabu | +irabu |
| +nyuma | +nyuma | +nyuma | +nyuma |
| +kati-juu | +kati-juu | +kati-chini | +kati-chini |
| +mviringo | +mviringo | +mviringo | +mviringo |
| | +urefu | | +urefu |

| [u] | [u:] | [i] | [i:] |
|---|---|---|---|
| +irabu | +irabu | +irabu | +irabu |
| +nyuma | +nyuma | +mbele | +mbele |
| +juu | +juu | +juu | +juu |
| +mviringo | +mviringo | -mviringo | -mviringo |
| | +urefu | | +urefu |

| [e] | [e:] | [I] | [I:} |
|---|---|---|---|
| +irabu | +irabu | +irabu | +irabu |
| +mbele | +mbele | +kati | +kati-mbele |
| +kati-juu | +kati-juu | +juu | +juu |
| -mviringo | -mviringo | -mviringo | -mviringo |
| | +urefu | | +urefu |

| [Ʊ] | [Ʊ:] |
|---|---|
| +irabu | +irabu |
| +kati-nyuma | +kati-nyuma |
| +juu | +juu |
| +mviringo | +mviringo |
| | +urefu |

Irabu za Kiarror zinaweza kuainishwa kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:


(i) Sehemu ya ulimi

(ii) Mwinuko wa ulimi

(iii) Mkao midomo

Kwa kuzingatia kigezo cha sehemu ya ulimi, irabu irabu huainishwa kama za mbele, irabu za katikati na irabu za nyuma. Kwa kuzingatia kigezo cha mwinuko wa ulimi, kuna irabu za juu, irabu za kati-juu, irabu za kati-chini na irabu ya chini. Ufuatao ni mchoro unaoonyesha irabu za Kiarror kwa kuzingatia mwinuko wa ulimi na sehemu ya ulimi.

**Kielelezo 2.5 Mchoro wa irabu za Kiarror**




Kigezo cha mkao wa midomo hubainisha irabu kwa kuzingatia kutandazwa au kuviringwa kwa midomo wakati wa utamkaji wake. Irabu zinazotamkwa huku midomo ikiwa imetandazwa ni /i/, /e/, /ɛ/, /I/ na /a/. Zile irabu zinazotamkwa huku midomo ikiwa imeviringwa ni /u/, /o/, /ʊ/ na /ɔ/. Kiwango cha kuviringwa au kutandazwa kwa midomo hutofautiana kulingana na irabu

inayohusika. Kwa mfano, wakati wa kutamkwa kwa irabu /a/, midomo hutandazwa zaidi kuliko inavyotandazwa wakati wa kutamka irabu /e/. Vile vile wakati wa kutamka irabu /o/, midomo huviringwa zaidi kuliko inavyoviringwa wakati wa utamkaji wa irabu /ɔ/.

Jedwali lifuatalo linaonyesha sifa bainifu za irabu za Kiarror. Sifa hizi zitatusaidia katika kuchanganua mifanyiko mbalimbali ya irabu.

**Jedwali 2.6 Sifa bainifu za irabu za Kiarror**

| Sauti / Sifa | I | I | e | ɛ | o | ɔ | a | u | ʊ |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Usilabi | + | + | + | + | + | + | + | + | + |
| Juu | + | + | - | - | - | - | - | + | + |
| Nyuma | - | - | - | - | + | + | - | + | |
| Chini | | | | | | | + | | |
| Mviringo | | | | | + | + | | + | + |
| Kaze | | | | | | | | | |
| Mbele | + | | + | + | | | | | |

Kiswahili tofauti na Kiarror, kina irabu tano ambazo ni: /a, ɛ, i, ɔ, u/. Irabu za Kiswahili huweza kutokea mwanzoni, katikati na mwishoni mwa silabi sawa na irabu za Kiarror. Katika Kiswahili, irabu za wakaa ndefu hudhihirika mwishoni mwa neno japo kuna maneno machache sana ya Kiswahili yanayotumia sifa ya wakaa kubainisha maana zao.

### 2.2.2 Konsonanti za Kiarror

Kiarror kina konsonanti kumi na moja pamoja na nusu irabu mbili. Konsonanti hizi ni: /p, t, ʧ, k, m, n, ɲ, ŋ, s, r, l/ nazo nusu irabu ni /j/ na /w/. Fonimu /p/ na /k/ zina alofoni ambazo hutokea kimpishano huru. Alofoni za [p] ni /p/ na /β/ kwa mfano, ingawa sauti tofauti zinatumika katika maneno haya: [bi:ʧ], [pi:ʧ] na [βi:ʧ], yote yanarejelea nomino 'watu'. Alofoni za [k] ni /k/, /g/ na /ɣ/ kwa mfano [kiriʧ], [giriʧ] na [ɣiriʧ] ni nomino zinazorejelea 'dawa'. Ingawa sauti tofauti zinatumika, maana ya neno halibadiliki. Silabi pendwa za Kiarror zina muundo wa KIK na KI: K. Muundo huu hufanya konsonanti na nusu-irabu kuweza kuchukua nafasi za mwanzo na mwisho katika silabi. Kwa mfano, katika neno [ko:rin], kuna silabi [rin] yenye mwanzo silabi na koda ambazo ni konsonanti /r/ na /n/ mtawalia. Kiarror pia huwa na konsonanti nazalishi. Hizi ni konsonanti ambazo huchukuliwa kama sauti moja zitamkwapo pamoja. Konsonanti nazalishi hutokea mwanzoni mwa silabi na zinaungana katika mazingira mahususi ambayo yanahusisha fonimu ya kwanza kuwa nazali, kisha inafuatawa na kipasuo (Mgullu 1999). Kiarror kina konsonanti nazalishi nne ambazo ni: /mb/, /nd/, /ŋg/ na /ɲɟ/

Jedwali lifuatalo linaonyesha uwakilishaji wa IPA na othografia ya konsonanti za Kiarror na maneno yanayotokeza konsonanti hizo.

**Kielelezo 2.7 Utambulisho wa konsonanti za Kiarror**

| **IPA** | **Othografia** | **Uwakilishi wa kifonetiki** | **maana** |
|---|---|---|---|
| /p/→[p], [β] | Put<br>Solop<br>chepto | [put]<br>[solop]<br>[ʧɛptɔ] | Bomoa<br>Mende<br>msichana |
| /t/ | Tany<br>otep<br>Iit | [taɲ]<br>[ɔtɛp]<br>[i:t] | Ng'ombe<br>Tabia<br>sikio |

| | | | |
|---|---|---|---|
| /k/→ [g], /k/, /ɣ/ | Koi<br>Kaat<br>Lokoi | [kɔi]<br>[ka:t]<br>[lɔ:ɣɔi] | Jiwe<br>Shingo<br>matunda |
| /s/ | Somok<br>Kasteen<br>Sok | [sɔmɔk]<br>[kastɛ:n]<br>[sɔk] | Tatu<br>Sikiliza<br>Majani |
| /ʧ/ | Chukui<br>Mecheei<br>Tech | [ʧuɣui]<br>[meʧɛ:i]<br>[teʧ] | Mbwa<br>Wifi<br>Kanyaga |
| /l/ | Laakwa<br>Muul<br>Kiplekwa | [la:kwa]<br>[mu:l]<br>[kiplɛkwa] | Mtoto<br>Iga<br>Sungura |
| /r/ | Reel<br>Reer<br>Rutoi | [re:l]<br>[re:r]<br>[rutɔi] | -eupe<br>Lia<br>Safari |
| /m/ | Mooi<br>Tuum<br>kumnyo | [mɔ:i]<br>[tu:m]<br>[kumɲɔ] | Ndama<br>Sherehe<br>Sima |
| /n/ | Nam<br>Yoosin<br>Kaina | [nam]<br>[jo:sin]<br>[kaina] | Shika<br>Uzee<br>jina |
| /ɳ/ | Ng'oom | [ɳɔ:m] | Mwerevu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Koong’o<br>Koong’ | [kɔ:ɳɔ]<br>[kɔ:ɳ] | Kumbekumbe<br>Jicho |
| /ɲ/ | Cheeny<br>Nyei<br>Konyen | [ʧɛ:ɲ]<br>[ɲei]<br>[kɔɲen] | Chukua<br>Tafuna<br>Macho |
| /j/ | Ya<br>Yey<br>Telya | [ja]<br>[jɛj]<br>[telja] | Mbaya<br>Fanya<br>rafiki |
| /w/ | Werto<br>Keweech<br>Keew | [wertɔ]<br>[kɛwɛ:ʧ]<br>[kɛ:w] | Mvulana<br>Tulime<br>Jangwa |
| /mb/ | Sember<br>Chumbiin | [sɛmbɛr]<br>[ʧumbi:n] | Palilia<br>Mzungu |
| /nd/ | Ndoi<br>Pendei | [ndɔ:i]<br>[pendei] | Tangulia<br>Wanaenda |
| /ɳg/ | Ngui<br>Kongoi | [ɳgui]<br>[koɳgoi] | Mboga<br>Asante |
| /ɳɟ/ | Munjurisyoon<br>Kilenjon | [muɲɟurisjɔ:n]<br>[kileɲɟɔ:n] | kungwi<br>Aliniambia |

### 2.2.2.1 Sifa bainifu za konsonanti za Kiarror

Kwa kutumia vigezo mbalimbali, konsonanti za Kiarror zinaweza kubainishwa ifuatavyo:

**(i) Vipasuo / Vizuiwa**

[p]

+kons
+kip
+mid
-naz
-ghuna

[t]

+kons
+kip
+ufz
-naz
-ghuna

[k]

+kons
+kip
+kkl
-naz
-ghuna

**(ii) Kipasuo- kwamizwa**

[ʧ]

+kon
+kkzw
+kkg
-naz
-ghuna

**(iii) Vikwamizwa**

[s]

| |
|---|
| +kons |
| +kmz |
| +ufizi |
| -naz |
| -ghuna |

| [ɣ] | [h] |
|---|---|
| +kons | +kons |
| +kmz | +kmz |
| +kkl | +glota |
| -naz | -naz |
| +ghuna | -ghuna |

**(iv) Nazali**

| [m] | [n] | [ɳ] | [ɲ] |
|---|---|---|---|
| +kons | +kons | +kons | +kons |
| +naz | +naz | +naz | +naz |
| +midomo | +ufizi | +kkl | +kkg |
| +ghuna | +ghuna | +ghuna | +ghuna |

**(v) Kitambaza**

[l]

| |
|---|
| +kons |
| +ktz |
| +ufizi |
| -naz |
| +ghuna |

**(vi) Kimadende**

**[r]**

+kons
+kmd
+ufizi
-naz
+ghuna

### 2.2.2.2 Nusu-irabu/ viyeyusho

Kuna nusu irabu mbili katika lugha ya Kiarror; /w/ na /j/. Nusu irabu hutamkwa kwa kuachilia hewa itokayo mapafuni ipitie chemba ya kinywa au chemba ya pua huku hewa ikitatizwa kidogo sana hivyo kusababisha mkwaruzo mdogo. Fonimu /w/ hutamkwa huku mdomo ukiwa mviringo nalo shina la ulimi likiwa limevutwa nyuma ukielekezwa kwenye kaakaa laini. Fonimu /j/ hutamkwa midomo ikiwa imetandazwa na bapa la ulimi likiwa limeinuliwa kuelekea kaakaagumu.

| [j] | [w] |
|---|---|
| +nusu irabu | +nusu-irabu |
| +kk gumu | +mid/kk laini |
| -naz | -naz |
| +ghuna | +ghuna |

**Uundaji wa nusu-irabu za Kiarror**

Kiarror kina nusu-irabu mbili ambazo ni /j/ na /w/. Nusu irabu hizi huundwa kutokana na kubadilika kwa irabu. Irabu zinazokumbwa na badiliko hili ni /i/ na /u/. Irabu hizi zikifuatwa na irabu ambazo ni tofauti nazo hubadilika kuwa nusu-irabu.

**Uundaji wa /j/**

Irabu /i/ hubadilika kuwa nusu-irabu /j/ katika mazingira ya kutangulia irabu isiyo /u/ au /i/ yenyewe. Sheria inayohusika ni:

/i/ ⟶ /j/ / _[irabu] (isiyo/u/ au /i/)

Kwa mfano:

(9 a) {ri +a:l} ⟶ { rja:l} ‘okota’

(9 b) {ir i+ɔ:ɲ} ⟶ { irjɔ:ɲ} ‘chemua’

Irabu /u/ hubadilika kuwa nusu-irabu /w/ katika mazingira ya kutangulia irabu isiyo /u/ yenyewe. Sheria inayohusika ni:

/u/ ⟶ /w/ ⁄ _ [irabu](isiyo /u/)

Kwa mfano:

(10 a) {ku+aɲ} ⟶ {kwaɲ} ‘songa sima’

(10 b) {ku+ɛi} ⟶ {kwɛi} ‘okota’

(10c) [ku+ɔɲ} ⟶ {kwɔɲ} ‘mwanamke’

**2.3 Fonimu za kiswahili**

Kwa mujibu wa Iribemwangi (2010), fonolojia ya konsonanti za Kiswahili ni suala ambalo limezua ubishani mkubwa miongoni mwa wanaisimu mbalimbali. Kuna maoni tofauti tofauti kuhusu idadi ya konsonanti za Kiswahili. Wanaisimu kama vile Kihore na wengine (2001) na Habwe na Karanja (2004) wanakubaliana kwamba Kiswahili kina konsonanti ishirini na tano ambazo ni /b, ʧ, d, ð, f, g, h, ɣ, ɟ, k, l, m, n, ɲ, ŋ, p, r, s, ʃ, t, θ, v, z,w, j/. Kwa upande mwingine, Iribemwangi (2010) anaeleza kuwa Kiswahili kina konsonanti ishirini na tano /b, ʧ, d, ð, f, g, h, ɣ, ɟ, k, l, m, ɱ, n, ɲ, ŋ, p, r, s, ʃ, t, θ, x, v, z/ pamoja na nusu irabu mbili /w, j/. huu ndio msimamo unaochukuliwa na utafiti huu. Wanaisimu wengine kama vile Mweri (2010) wanadai kuwa Kiswahili kina konsonanti thelathini na mbili.

Sababu zinazoibua tofauti kimaoni kuhusu konsonanti za Kiswahili ni kwamba kuna wanaisimu wanaotambua konsonanti nazalishi kama fonimu mahususi inayoweza kujisimamia kama vile Mweri (2010) na kuna wale wasiotambua konsonanti nazalishi kama fonimu mahususi kama vile Mwaliwa (2014). Mifano ya konsonanti nazalishi ni kama vile: /nd, mb, nz, nɟ, nt, nʧ/ Mgullu (1999). Aidha, maoni tofauti ya wataalamu mbalimbali kuhusiana na idadi ya konsonanti za

Kiswahili ni kutokana na nafasi za konsonanti za Kiswahili zenye asili ya kigeni kama vile konsonanti /x/. Mwaliwa (2014) anaeleza kuwa, konsonanti /x/ si fonimu ya Kiswahili kwa sababu haina uwezo wa kutofautisha maana katika maneno ya Kiswahili. Badala yake, inabainisha tu maana katika maneno yenye asili ya Kiarabu.

Tofauti na konsonanti, idadi ya fonimu za irabu za Kiswahili haijazua utata mwingi. Wataalamu wengi kama vile Mgullu (1999), Iribemwangi (2010, Mwaliwa (2014) na wengine wanaafikiana kuwa Kiswahili kina fonimu tano za irabu ambazo ni /a/, /e/, /i/, /ɔ/ na /u/. Irabu hizi hubainishwa kwa vigezo vitatu vikuu; sehemu ya ulimi, mwinuko wa ulimi na mkao wa mdomo.

### 2.3 Muundo wa silabi katika Kiarror

Obuchi na Mukhwana (2015) wanaeleza kuwa silabi ni kipashio cha kifonolojia kinachohusu matamshi na ambacho kwacho sauti za lugha hutamkwa mara moja kama fungu moja linalojitegemea. Hivyo basi, mara nyingi silabi husheheni sauti moja, mbili au zaidi na huundwa kwa konsonanti, irabu au mwambatano wa konsonanti na irabu. Muundo wa silabi hutegemea lugha husika. Crystal (1991) anaifafanua silabi kama kipashio cha kimatamshi ambacho ni kikubwa kuliko fonimu, lakini kidogo kuliko neno. Aidha, silabi inaweza kuwa sauti moja ambayo hutamkwa pekee katika mazingira fulani ya neno. Kila lugha huwa na mfumo wake wa silabi zenye miundo tofauti tofauti. Hooper (1972) anasisitiza kuwa ni muhimu kuelewa mfumo wa silabi katika lugha kwa sababu mfumo wa lugha huwa muhimu katika kuchanganua mifanyiko ya kifonolojia kwa vile mabadiliko ya sauti aghalabu hutokea kutegemea ujirani wa sauti moja na nyingine. Kuna aina mbili kuu za silabi; silabi wazi na silabi funge.

#### 2.3.1 Silabi wazi

Hyman (1975), Ladefoged (1975) na O’Grady (1997) wanaeleza kuwa silabi wazi haina koda. Clements na Keyser (1983) wanatoa maelezo kuwa lugha zote zina muundo huu wa silabi. Silabi wazi ni zile ambazo huishia kwa irabu. Matamshi ya silabi wazi huendelezwa polepole wala hayakatizwi ghafla. Silabi pendwa katika Kiswahili ni silabi wazi na hudhihirika katika mifano ifuatayo ya maneno:

(11 a) [ka$la$mu]

(11 b) [mɛ$za]

(11 c) [ða$ha$bu]

Silabi wazi katika Kiarror huwa chache. Katika mchakato wa utohozi wa maneno mkopo kutoka Kiswahili, aghalabu Kiarror huweka koda katika neno mkopo lisilokuwa na koda ili kuifanya silabi ya mwisho kuwa funge. Ifuatayo ni mifano ya maneno ya Kiarror yaliyo na silabi wazi:

(12 a) [la:$kwa] ‘mtoto’

(12 b) [ʧɛpjɔ:$sɔ] ‘mwanamke’

(12 c) [mɔ:$] ‘tumbo’

**2.3.1.1 Miundo ya silabi wazi katika Kiarror**

Hyman (1975) anaeleza kwamba kila lugha huwa na muundo wake wa silabi. Ingawa kuna baadhi ya silabi za Kiarror zinazofanana kimuundo na silabi za Kiswahili, silabi nyingi za Kiarror zinatofautiana kimuundo na silabi za Kiswahili.

**(i) Muundo wa irabu pekee (I)**

Kiarror kina irabu fupi zinazoweza kusimama kama silabi katika neno bila kuandamana na koda wala mwanzo. Muundo huu huweza kutokea mwanzoni mwa neno. Maneno yafuatayo yanaonyesha muundo huu wa silabi:

(13 a) [**i**$bɔt] anguka

(13 b) [**a**$mi:] nipo

(13 c) [**a**$pa] nendeni

**(ii) Muundo wa irabu ndefu pekee (I:)**

Huu ni muundo unaohusisha irabu moja ya wakaa ndefu. Muundo huweza kutokea mwanzoni au katikati mwa neno. Kwa mfano:

(14 a) [**i:**$ti:] sikio

(14 b) [**ɛ:**$un] mikono

(14 c) [**ɛ:**] ndiyo

Silabi zilizokolezwa wino ndizo zinazodhihirisha muundo wa irabu ndefu pekee.

**(iii) Muundo wa konsonanti, irabu ndefu (KI:)**

Huu ni muundo unaoundwa kwa konsonanti moja na irabu moja yenye wakaa ndefu. Huweza kutokea mwanzo au katikati ya neno. Kwa mfano:

(15 a) [e$**mɔ:]** salamu

(15 b) [**pa:**$ndɛ] mahindi

(15 c) [ʧe:$**mɔ:**$si] jitu

Silabi zilizokolezwa wino ndizo zinazodhihirisha muundo wa konsonti moja na irabu ndefu.

**(iv) Muundo wa konsonanti, nusu irabu, irabu ($K^{1}/_{2}II$)**

Muundo huu unahusisha konsonanti moja, nusu irabu moja na irabu moja ya wakaa fupi. Ni muundo unaoweza kutokea tu mwishoni mwa neno. Kwa mfano:

(16 a) [ki$**tjɔ**] pekee

(16 b) [te$**lja**] rafiki

(16 c) [la:$**kwa**] mtoto

Silabi zilizokolezwa wino ndizo zilizo na muundo wa konsonanti, nusu irabu na irabu.

**(v) Muundo wa konsonanti, nusu irabu, irabu ndefu ($K^{1}/_{2}II:$)**

Muundo huu huhusisha konsonanti moja, nusu irabu moja na irabu moja ya wakaa ndefu. Silabi hii inaweza kutokea popote katika neno. Kwa mfano:

(17 a) [**kwɔ:**$ɲ] mwanamke

(17 b) [i$**tjɔ:**$run] piga teke

(17 c) [ʧɛ$**pjɔ:**$sɔ] mwanamke

Silabi zilizoandikwa kwa wino uliokolezwa ndizo zilizo na muundo wa konsonanti, nusu irabu na irabu ya wakaa ndefu ndefu.

### 2.3.2 Silabi funge

Silabi funge ni silabi ambazo huwa na koda. Silabi hizi zinaweza kuwa na mwanzo silabi au zinaweza kukosa kuwa na mwanzo silabi. Silabi funge ni zile silabi zilizo na konsonanti mwishoni. Matamshi ya silabi funge hukatizwa ghafla. Katika Kiswahili, silabi hizi huwa chache na ni zile zinazounda maneno yaliyokopwa ila katika Kiarror, silabi za aina hii huwa nyingi. Ifuatayo ni mifano ya maneno ya Kiswahili yanayodhihirisha silabi funge:

(18 a) [**muh**$tasari]

(18 b) [**tas**$limu]

(18 c) [**muk**$taða]

Mifano ifuatayo ya maneno ya Kiarror hudhihirisha silabi funge:

| | |
|---|---|
| (19 a) [**ʧɛ:p**ka:**met**] | ‘dada’ |
| (19 b) [a$**ɳɛ:r**] | ‘ngumu’ |
| (19 c) [**mu:t**$] | ‘tano’ |

#### 2.3.2.1 Miundo ya silabi funge katika Kiarror

**(i) Muundo wa konsonanti, irabu, konsonanti (KIK)**

Hii ndiyo silabi pendwa katika Kiarror. Muundo huu huhusisha konsonanti moja, irabu moja yenye wakaa fupi na konsonanti moja. Muundo huu huweza kutokea pahali popote katika neno. Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| (20 a) $**sot**$ | kibuyu |
| (20 b) [sɔ$**sɔm**] | thelathini |
| (20 c) [**taɲ**$] | ng’ombe |

**(ii) Muundo wa konsonanti, irabu ndefu, konsonanti (KI:K)**

Muundo huu unahusisha konsonanti moja, irabu moja ya wakaa ndefu na irabu moja. Silabi hii huweza kutokea sehemu yoyote katika neno. Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| (21 a) [$**ʧi:ʧ**$] | mtu |
| (21 b) [**mu:t**$] | tano |
| (21 c) [sum$**ɲɔ:n**] | uchafu |

**(iii) Muundo wa irabu, konsonanti (IK)**

Muundo huu ni wa irabu moja fupi na konsonanti moja. Silabi hii hutokea mwanzoni mwa neno. Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| (22 a) [**ar**$ta] | mbuzi |
| (22 b) [**al**$dɛ:n] | uza |
| (22 c) [am$] | kula |

**(iv) Muundo wa irabu ndefu, konsonanti (I:K)**

Muundo huu unahusisha irabu moja ya wakaa ndefu na konsonanti moja. Silabi hizi zinaweza kutokea mwanzoni au mwishoni mwa neno. Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| (23 a) [**u:r**$wɔ] | kivuli |
| (23 b) [**i:t$**] | sikio |
| (23 c) [**ɔ:n**$] | fukuza |

**(v) Muundo wa konsonanti, nusu irabu, irabu, konsonanti (K½IIK)**

Silabi zenye muundo huu huundwa kwa konsonanti moja, nusu irabu moja, irabu moja ya wakaa fupi na konsonanti moja. Muundo huu unaweza kutokea pahali popote katika neno. Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| (24 a) [**kwer**$] | gonga |
| (24 b) [**kwɛ**t$] | kukatiza |
| (24 c) [**mwɛt**] | safisha |

### (vi) Muundo wa konsonanti, nusu irabu, irabu ndefu, konsonanti (K$^{1}/_{2}$II:K)

Silabi zenye muundo huu huundwa kwa konsonanti moja, nusu irabu moja, irabu moja ya wakaa ndefu na konsonanti moja. Ni muundo unaoweza kutokea pahali popote katika neno. Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| (25 a) [ɳɔ$**ljɔ:n**] | neno |
| (25 b) [tu$wo$**ljɔ:n**] | kengele |
| (25 c) [a$**kwa:n**] | njooni |

## 2.4 Silabi za Kiswahili

Muundo wa silabi za Kiswahili ni tofauti na ule wa Kiarror. Wanaisimu mbalimbali wanakubaliana kuwa Kiswahili kina miundo ya silabi ya KI na I. Silabi pendwa ya Kiswahili ni KI. Silabi KI na I katika Kiswahili hupatikana kwa maneno ya kiasilia, Mwaliwa (2014). Kwa mujibu wa Mgullu (1999), kiswahili pia kina miundo ya KIK na IK ambayo hutokana na maneno mkopo. Kijumla, Kiswahili kina silabi msingi KI, I, KIK na IK. Iribemwangi (2010) anaeleza kuwa pia Kiswahili kina miundo ya silabi ya KKI ambayo huundwa kwa konsonanti mbili na irabu, KK$^{1}/_{2}$II ambayo huundwa kwa konsonanti mbili nusu irabu na irabu, K ambayo huundwa kwa konsonanti moja pekee, KII ambayo huundwa kwa konsonanti moja na irabu ndefu na KKKI ambayo huundwa kwa konsonanti tatu na irabu moja. Muundo wa KKKI ni muundo unaopatikana tu katika maneno mkopo.

## 2.5 Hitimisho

Sura hii imebainisha kuwa mifumo ya kifonolojia ya Kiswahili na Kiarror inatofautiana kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, kuna fonimu zinazopatikana katika Kiswahili lakini hazipatikani katika Kiarror kama vile /h/, /f/, /v/ na /θ/, na kuna zile zinazopatikana katika Kiarror ila hazipatikani katika Kiswahili mathalan /β/ na /ʊ/. Kwa kuzingatia silabi, Kiswahili huruhusu mwambatano wa konsonanti mwanzoni mwa neno lakini Kiarror hakiruhusu. Sura hii ni muhimu katika kutuwezesha kuelewa jinsi Kiarror kinavyoshughulikia tofauti hizi ili kuruhusu maneno mkopo yakubalike katika mfumo wake wa kimofofonolojia.

## SURA YA TATU

## UTOHOZI KIFONOLOJIA WA MANENO MKOPO YA KIARROR KUTOKA KISWAHILI

### 3.1 Utangulizi

Katika sura ya pili, tulielezea fonolojia vipande sauti ya Kiarror na Kiswahili. Aidha, ufafanuzi wa miundo ya silabi za Kiswahili na Kiarror ulitolewa. Uchanganuzi huo ndio unaoweka msingi wa uchanganuzi wa utohozi wa kifonolojia wa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili. Kang' (2010) anaeleza kuwa lugha ikikopa maneno, ni sharti maneno hayo yatoholewe ili yaweze kuingiliana na mfumo wa kiisimu wa lugha pokezi. Maneno ya Kiswahili yanapoingizwa katika leksimu ya Kiarror, huwa na mfumo wa kimofofonolojia wa Kiswahili. Wasemaji wa Kiarror huyatohoa maneno hayo ili yaingie katika mfumo wa kimofofonolojia wa Kiarror. Mabadiliko hufanywa katika konsonanti, irabu na miundo ya silabi za maneno yanayokopwa. Katika sura hii, mifanyiko ya konsonanti na irabu katika maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili ilifafanuliwa. Kanuni za kifonolojia pia zikaonyeshwa kwa kutumia nadharia ya fonolojia zalishi asilia ili kuelezea mifanyiko hiyo.

### 3.2 Utohozi wa irabu

Kuna tofauti kati ya idadi ya irabu za Kiarror na za Kiswahili. Ilibainika kuwa irabu za Kiarror zinajitokeza katika jozi ambapo kila jozi hujumuisha irabu fupi na irabu ndefu. Kijumla, Kiarror kina irabu kumi na nane tofauti na Kiswahili ambacho kina irabu tano pekee. Aidha, utafiti wetu ulibainisha kuwa irabu zote tano za Kiswahili zinapatikana katika Kiarror. Ingawa mchakato wa utohozi wa maneno mkopo unaweza kuhusisha udumishaji wa irabu kama vile katika neno /paɲga/ 'panga (kifaa cha kukatia)', baadhi ya irabu hubadilika kifonetiki kwa sababu ya kimazingira kama ilivyo katika mchakato wa uwiano wa irabu, kulifanya neno liweze kukubalika katika mfumo wa kimofofonolojia wa Kiarror au kwa ajili ya kurahisisha matamshi ya neno. Baadhi ya mifanyiko ya kifonolojia inayokumba irabu za maneno mkopo ni udondoshaji wa irabu, uchopekaji wa irabu, uwiano wa irabu, uyeyushaji na urefushaji wa irabu. Utohozi wa irabu huweza kuchochewa na mfumo wa kifonolojia wa Kiarror au mfumo wa kimofolojia wa Kiarror.

### 3.2.1 Udondoshaji wa irabu

Udondoshaji ni hali ambapo kipashio kinachounda neno; irabu, konsonanti au silabi hutoweka kabisa kwenye mazingira maalum ya kifonolojia au ya kimofofonolojia. Mfanyiko huu unahusishwa sana na muundo mwafaka wa silabi (Schane 1973). Mchakato wa utohozi wa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili unahusisha kudondoshwa kwa irabu ili neno likubalike katika mfumo wa kimofofonolojia wa Kiarror. Utafiti wetu ulibainisha kuwa udondoshaji wa irabu hutokea kwa njia zifuatazo: Kwanza, Kiarror huweza kudondosha irabu iliyo katikati mwa konsonanti mbili. Ikiwa neno lina irabu baina ya kipasuo /t/ na kimadende /r/ au baina ya kipasuo /k/ na kimadende /r/, basi irabu hiyo hudondoshwa kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (32 a) /kar**a**tasi/ | [kartasi] |
| /a/ ⟶ [ø] / | /r/ __ /t/ |
| (32 b) /sɛr**i**kali/ | [sɛrɣali] |
| /a/ ⟶ [ø] / | /r/ __ /ɣ/ |
| (32 c) /kɔr**ɔ**kɔrɔni/ | [kɔrkɔrɛː] |
| /ɔ/ ⟶ [ø] / | /r/ __ /k/ |

Kanuni jumlishi ya mabadiliko haya ni:

$$\begin{pmatrix} \text{+irabu} \end{pmatrix} \longrightarrow [\text{ø}] \;/\; \begin{pmatrix} \text{+kons} \\ \text{+kmd} \\ \text{+ufz} \\ \text{-naz} \\ \text{+ghn} \end{pmatrix} ___ \begin{pmatrix} \text{+kons} \\ \text{-naz} \end{pmatrix}$$

Badiliko la aina hii huhamasishwa na mfumo wa Kiarror wa kifonolojia kwa sababu lengo lake ni kuafikiana na muundo wa silabi pendwa ya Kiarror ambayo ni KIK. Silabi ya kwanza katika maneno haya ina muundo wa KIK, yaani, neno la Kiswahili #**ka**$ra$ta$si# linageuka kuwa #**kar**$ta$si#, #**sɛ**$ri$ka$li# linageuka kuwa #**sɛr**$ɣa$li# na #**kɔ**$rɔ$kɔ$rɔ$ni# linageuka kuwa #**kɔr**$ɣɔ$rɛ:#.

Utafiti huu pia ulibainisha kwamba Kiarror hudondosha irabu zilizo mwishoni mwa nomino mkopo. Udondoshaji huu hufanyika ili kufanya neno likubalike katika mfumo wa kifonolojia wa Kiarror kwa kuafiki muundo wa silabi KIK. Irabu /i/ iliyoko mwishoni mwa neno mkopo hudondoshwa ili kuunda silabi funge KIK ambayo Kiarror hupendelea, kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (33 a) /lam**i**/ | [la:m] |
| (33 b) /nafas**i**/ | [napa:s] |
| (33 c) /kabat**i**/ | [kapat] |

/i/ ⟶ [ø] / [+kons] __#

Kanuni:

$$\begin{bmatrix} +irabu \\ +silabi \end{bmatrix} \longrightarrow [ø] \; / \; \begin{bmatrix} +kons \end{bmatrix} __\#$$

Udondoshaji husababisha neno [la$mi] lenye silabi mbili kugeuka kuwa na silabi moja #la:m# na neno #na$fa$si# lenye silabi tatu hupoteza silabi yake ya tatu kupitia udondoshaji wa /i/ na kuwa na silabi mbili #na$pa:s#. Aidha, neno la Kiswahili #ka$ba$ti# hubadilika na kuwa na silabi mbili #ka$pat#.

Kiarror pia hudondosha irabu mwanzoni mwa nomino mkopo dhahania zinazoanza na irabu /u/ kama ifuatavyo:

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (34 a) /**u**taɟiri/ | [taʧi:rnɔt] |
| (34 b) /**u**dɛrɛva/ | [ndɛrɛpainɔt] |
| (34 c) /**u**sta:rabu/ | [starapainɔt] |

/u/ ⟶ [ø] / __ /K/

Kanuni:

[+irabu, +usilabi] ⟶ [ø] / [+kons, # __] -sila

Mfanyiko huu wa kifonolojia hutokea kwa sababu za uambishaji wa kimofolojia wa nomino za Kiarror kwani Kiarror aghalabu huambisha mofimu {nɔt} mwishoni mwa mzizi wa nomino ili kudhihirisha udhahania wake. Uambishaji huu huongeza idadi ya silabi kwenye nomino husika. Ili kusahilisha utamkaji wa nomino husika kwa kuepuka uziada, Kiarror hudondosha irabu ya mbele /u/ katika nomino mkopo dhahania inayoanza na /u/.

### 3.2.2 Uchopekaji wa irabu

Kanuni za usilabishaji katika fonolojia ya Kiarror haziruhusu mwambatano wa konsonanti /mʃ/, /mk/ na /mʧ/ mwanzoni mwa nomino. Aidha, fonolojia ya Kiarror haina muundo wa silabi yenye konsonanti pekee. Kwa sababu hiyo, wasemaji wa Kiarror hujaribu kutafuta jinsi ya kurahisisha utamkaji wa nomino mkopo zinazoanza na konsonanti zilizo na usilabi kama vile nazali ya mdomo /m/. Hivyo basi, irabu huchopekwa kati ya konsonanti mbili ili kuunda silabi yenye konsonanti na irabu. Mifano ifuatayo inadhihirisha hali hii.

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (35 a) /mʃahara/ | /m**u**sjara/ |
| (35 b) /mkatɛ/ | /m**a**ɣatja:n/ |
| (35 c) /mʧɛlɛ/ | /m**u**ʧele/ |

/ø/ ⟶ [irabu] / [kons]__[kons]

Kanuni ifuatayo inadhihirisha mchakato huu:

$$/\text{ø}/ \longrightarrow \begin{bmatrix} \text{+sila} \\ \text{-kons} \end{bmatrix} \Big/ \begin{bmatrix} \text{+kons} \\ \text{+sila} \\ \text{+naz} \\ \text{+mid} \end{bmatrix} ___ \begin{bmatrix} \text{+kons} \\ \text{-sila} \end{bmatrix}$$

### 3.2.3 Uyeyushaji

Uyeyushaji ni badiliko linalohusu kuimarika kwa irabu kuwa nusu irabu. Badiliko hili hutokea irabu mbili zikifuatana katika mazingira yasiyoruhusiwa katika Kiarror. Irabu /i/ au /u/ ikitangulia irabu /a/, katika mazingira ya kufuatana moja kwa moja, irabu tandaze ya juu, mbele /i/ huimarika na kuwa kiyeyusho /j/, nayo irabu viringe /u/ ya juu nyuma huimarika na kiyeyusho /w/. Lengo la uyeyushaji katika Kiarror ni kupata muundo mwafaka wa silabi ya konsonanti, nusu irabu, irabu (K$^{1/}{}_{2}$II). Mifano ifuatayo inadhihirisha uyeyushaji wa irabu /u/ na /i/ katika nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili.

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (36 a) /barua/ | /par**w**a/ |

/u/ ⟶ /w/ / __ [irabu ] (isiyo /u/)

Kanuni:

$$\begin{bmatrix} \text{+irabu} \\ \text{+juu} \\ \text{+nyuma} \end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix} \text{+nusu irabu} \\ \text{+mid/kklaini} \\ \text{-naz} \\ \text{+ghn} \end{bmatrix} \Big/ ___ \begin{bmatrix} \text{a} \\ \text{ɛ} \\ \text{i} \\ \text{ɔ} \end{bmatrix}$$

| | |
|---|---|
| (36 b) /sufuria/ | /supur**y**ɔ/ |
| (36 c) /ʃɛria/ | /sɛr**j**aː/ |

/i/ → /j/ / __ [irabu] (isiyo /i/)

Kanuni:

$$\begin{bmatrix}\text{+irabu}\\ \text{+juu}\\ \text{+mbele}\end{bmatrix} \rightarrow \begin{bmatrix}\text{+nusi irabu}\\ \text{+kkgumu}\\ \text{-naz}\\ \text{+ghn}\end{bmatrix} / __ \begin{bmatrix}\text{a}\\ \text{ɛ}\\ \text{ɔ}\\ \text{u}\end{bmatrix}$$

### 3.2.4 Uwiano wa irabu

Huu ni mchakato wa kiusilimisho ambapo irabu moja huathiriwa na irabu nyingine iliyo jirani yake. Irabu zinazoathiriana husababishwa kukubaliana kwa kiasi cha kuinuliwa kwa ulimi, mkao wa mdomo wakati wa kutamkwa na ikiwa irabu inatamkiwa mbele au nyuma. Michakato ya uwiano wa irabu hutokea wakati irabu mbalimbali zinaathiriana kisifa. Mchakato wa uwiano wa irabu hupata motisha kutokana na haja ya kuleta ukubalifu wa kifonolojia na urahisishaji wa matamshi. Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa katika maongezi ya kawaida, sauti hazitolewi kama mfuatano wa sauti huru zinazojitegemea, bali kama msuko wa sauti zinazoingiliana. Hii ina maana kuwa sauti huathiriana kulingana na sifa zao. Mifano ifuatayo inadhihirisha hali hii inavyotokea katika utohozi wa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili.

Irabu /u/ huweza kubadilika na kuwa irabu /ɔ/ katika neno ikitokea katika mazingira ya kukaribiana na irabu /a/ mathalan:

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (38 a) /r**u**husa/ | /r**ɔ**sa/ |
| (38 b) /k**u**ra/ | /k**ɔ**ra/ |
| (38 c) /hɛsab**u**/ | /ɛsa:p**ɔ**/ |

Irabu /u/ hutamkiwa juu, irabu /ɔ/ hutamkiwa katikati nayo irabu /a/ hutamkiwa chini. Irabu /ɔ/ inakaribiana kifonolojia na irabu /a/ kuliko ilivyo irabu /u/. Hii ndio maana irabu /u/ inabadilika kuwa /ɔ/ katika mazingira ya kukaribiana na irabu /a//

Irabu /i/ aidha huweza kubadilika na kuwa irabu /e/, kwa mfano:

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (39 a) /mp**i**ra/ | /mb**e**ra/ |
| (39 b) /ʃ**i**da/ | /s**e**:ta/ |
| (39 c) /d**i**r**i**ʃa/ | /t**e**r**e**sja/ |

Irabu /e/ ambayo hutamkiwa kati juu hukaribiana kifonetiki na irabu /a/ kuliko ilivyo irabu /i/ inayotamkiwa juu, kwa hivyo ni rahisi kuitamka /e/ iliyo katika mazingira yaliyo karibu kifonolojia na /a/ kuliko kuitamka /i/ katika mazingira yanayokaribiana na /a/.

### 3.2.5 Urefushaji wa irabu

Tofauti na Kiswahili, Kiarror huwa na aina mbili za irabu; irabu fupi na irabu ndefu. Utohozi wa baadhi ya maneno yanayokopwa kutoka Kiswahili huhusu urefushaji wa irabu. Kiarror hurefusha irabu katikati mwa nomino mkopo ili kufidia ile irabu inayodondoshwa mwishoni mwa nomino yenyewe katika kuunda silabi funge ya KIK inayopendelewa na Kiarror. Mfanyiko huu hutokea kama ifuatavyo:

/i/ ⟶ [i:] / [kons]__[kons]

Mifano ya nomino mkopo zinazoonyesha mfanyiko huu ni:

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (41 a) /naf**a**si/ | /nap**a:**s/ |
| (41 b) /m**a**ndazi/ | /mand**a:**s/ |
| (41 c) /b**a**fu/ | /p**a:**p/ |

### 3.3 Utohozi wa konsonanti

Ingawa konsonanti nyingi za Kiswahili zinapatikana katika Kiarror, kuna baadhi yazo ambazo hazipatikani katika kiarror kama vile vikwamizo /θ/, /h/ na / ð/. Katika mchakato wa utohozi wa konsonanti za nomino mkopo, kukosekana kwa konsonanti hizi katika fonolojia ya Kiarror hufidiwa na kuimarishwa au kudhoofishwa kwa konsonanti hizi. Pia, konsonanti zinaweza

kudondoshwa na nafasi yake kuachwa wazi au irabu inaweza kurefushwa ili kufidia kukosekana kwa konsonanti iliyodondoshwa. Mifanyiko mbalimbali ya kifonolojia hutokea katika konsonanti za nomino mkopo zinazotoholewa. Mifanyiko hiyo ni kama vile kuimarika na kudhoofika kwa konsonanti, kuchopekwa na kudondoshwa kwa konsonanti na ubadala wa konsonanti. Mifanyiko ya kifonolojia katika utohozi wa nomino mkopo mara nyingi huchochewa na tofauti za mifumo ya kimofolojia ya Kiswahili na Kiarror. Aidha, mifanyiko inaweza kuchochewa na jaribio la kurahisisha matamshi ya nomino.

### 3.3.1 Kuimarika na kudhoofika kwa konsonanti

Mgullu (1999) anaeleza kwamba nguvu ambazo mtu hutumia anapotamka konsonanti mbalimbali zinatofautiana kutegemea aina za konsonanti anazozitamka. Zipo konsonanti zinazohitaji nguvu nyingi wakati wa kutamka na zipo zinazohitaji nguvu kidogo. Sauti za lugha hupangwa kwa kutegemea nguvu inayotumika katika kuzitamka. Ni kwa msingi huu ndipo tunapopata orodha ifuatayo:

(i) Vipasuo visoghuna k.m /p/, /t/, /k/
(ii) Vipasuo ghuna k.m /b/, /d/, /g/
(iii) Vipasuo kwamizo visoghuna k.m /ʧ/
(iv) Vipasuo kwamizo ghuna k.m /ɟ/
(v) Vikwamizo visoghuna k.m /f/, /s/, /θ/. /ʃ/
(vi) Vikwamizo ghuna k.m /v/, /z/, / ð/
(vii) Nazali k.m /m/, /n/, /ɳ/, /ɲ/
(viii) Vimadende k.m /r/
(ix) Vitambaza k.m /l/
(x) Nusu irabu k.m /j/, /w/
(xi) Irabu k.m /a/, /ɛ/, /i/, /ɔ/, /u/

Orodha hii ina ngazi kumi na moja ambapo ya kwanza huhusisha matumizi ya nguvu nyingi katika utamkaji ilhali ya kumi na moja huhusisha matumizi ya nguvu kidogo zaidi. Kutokana na orodha hii, inadhihirika kuwa sauti zisizokuwa na mghuno hutamkwa kwa kutumia nguvu nyingi zaidi kuliko zile zenye mghuno.

#### 3.3.1.1 Kuimarika kwa konsonanti

Kuimarika kwa konsonanti hutokea pale ambapo alofoni za sauti fulani hutamkwa kwa nguvu nyingi kuliko sauti yenyewe. Badiliko la aina hii huwa ni la kimazingira. Baadhi ya konsonanti za Kiswahili zinapokopwa na kutoholewa katika Kiarror huimarika kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

**(i) Kikwamizo (-ghuna) kuwa kipasuo (-ghuna)**

Vikwamizo hutamkwa kwa kutumia nguvu kidogo vikilinganishwa na vipasuo. Vikwamizo hafifu vinavyohusishwa na mfanyiko huu na /f/ na /θ/. Kwa kuwa konsonanti /f/ ambayo hutamkiwa katika mdomo-meno haipo katika fonolojia ya Kiarror, konsonanti hii huimarika kuwa /p/ ambayo hutamkiwa kwenye midomo ili kuifanya ikubalike katika mfumo wa kifonolojia wa Kiarror.

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (42 a) /**f**undi/ | /**p**undi/ |
| (42 b) /ba**f**u/ | /pa:**p**/ |
| (42 c) /**f**ilimbi/ | /**p**irimbi/ |

/f/ ⟶ [p] / __ [irabu]

Vilevile, konsonanti /θ/ hubadilika kuwa /t/ kwa sababu /θ/ haipo katika mfumo wa kifonolojia wa Kiarror kwa hivyo ni sharti itafutiwe kibadala ambacho ni kina ukuruba na /θ/ na kwa vile /θ/ hutamkiwa meno, na fonolojia ya Kiarror haina sauti za meno, basi sauti inayotamkiwa katika ala inayokaribiana na meno (ufizi) huchaguliwa. Kwa mfano:

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (43 a) /**θ**ɛluɟi/ | /**t**ɛluʧi/ |
| (43 b) /**θ**ɛmanini/ | /**t**amanini/ |
| (43 c) /**θ**ibitiʃɔ/ | /**t**ipitisjɔ/ |

/θ/ ⟶ [t] / __ [irabu]

Sheria ya kijumla kwenye mabadiliko haya ni:

$$\begin{bmatrix} \text{+kmz} \\ \text{-mgh} \\ \text{+kont} \end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix} \text{+kip} \\ \text{-mgh} \\ \text{-kont} \end{bmatrix} \Big/ __ \begin{bmatrix} \text{+sila} \\ \text{-kons} \end{bmatrix}$$

**(ii) Kikwamizo (+ghuna) kuwa kipasuo (-ghuna)**

Badiliko hili linahusisha konsonanti /v/ ya mdomo-meno ambayo hubadilika kuwa konsonanti /p/ ya midomo. Aidha, inahusisha konsonanti /ɣ/ ya kaakaa laini ambayo hubadilika kuwa konsonanti /k/. konsonanti /v/ haipo katika mfumo wa kifonolojia wa Kiarror, kwa hivyo, inapaswa kuimarishwa iwe /p/ ili ikubalike katika mfumo wa kifonolojia wa Kiarror, kwa mfano:

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| /v/ → /p/ | |
| (44 a) /**v**iazi/ | /**p**iasi/ |
| (43 b) /**v**uɲɟa/ | /**p**oɲʧan/ |
| (44 c) /**v**ɛranda/ | /**p**ɛranda/ |

/v/ ⟶ [p] ╱ __ [irabu]

/ɣ/ ⟶ /k/

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (45 a) /**ɣ**arama/ | /**k**arama/ |
| (45 b) /**ɣ**ɔrɔfa/ | /**k**ɔrɔpa/ |
| (45 c) /**ɣ**asia/ | /**k**asija/ |

/ɣ/ ⟶ [k] ╱ __ [irabu]

Sheria ya kijumla kwenye mifanyiko hii ni:

$$\begin{bmatrix} +\text{kons} \\ +\text{kmz} \\ +\text{mgh} \\ +\text{kont} \end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix} +\text{kons} \\ +\text{kip} \\ -\text{mgh} \\ -\text{kont} \end{bmatrix} \Big/ ___ \begin{bmatrix} +\text{sila} \\ -\text{kons} \end{bmatrix}$$

**(iii) Kipasuo (+ghuna) kuwa kipasuo (-ghuna)**

Mifanyiko hii huhusisha konsonanti ghuna /d/ ya ufizi inayobadilika kuwa konsonanti sighuna /t/ ya ufizi, konsonanti ghuna /b/ ya midomo kubadilika kuwa konsonanti sighuna /p/ ya midomo na konsonanti ghuna /g/ ya kaakaa laini ambayo hubadilika kuwa konsonanti sighuna /k/ ya kaakaa laini. Mifano ifuatayo inaonyesha mabadiliko ya maneno mkopo ya kiarror yanayokopwa na kutoholewa kutoka Kiswahili.

**(a) Kuimarika kwa /d/ kuwa /t/**

Konsonanti /d/ na /t/ zina uhusiano wa karibu sana wa kifonetiki kwani zote ni vipasuo ambavyo hutamkiwa kwenye ufizi. Tofauti ni kwamba /d/ ni kipasuo ghuna ila /t/ ni kipasuo sighuna. Katika Kiarror, konsonanti /d/ haiwezi kutokea katika mazingira ya kutanguliwa na kufuatwa na irabu moja kwa moja bali huweza tu kutumiwa katika kuunda konsonanti nazalishi /nd/ kama katika neno /tɛndɛn/ (-embamba). Kwa mantiki hiyo, maneno mkopo kutoka Kiswahili yaliyo na konsonanti /d/ inayojisimamia yanapotoholewa, konsonanti /d/ huimarishwa kuwa konsonanti /t/ ili yakubalike katika fonolojia ya Kiarror. Kwa mfano:

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (46 a) /**d**ini/ | /**t**ini/ |
| (46 b) /**d**akika/ | /**t**aɣika/ |
| (46 c) /**d**araɈa/ | /**t**araʧ/ |

$$/d/ \longrightarrow [t] \;\big/\; __ \;[\text{irabu}]$$

**(b) Kuimarika kwa /b/ kuwa /p/**

Konsonanti yenye mghuno /b/ hutumiwa kama alofoni ya konsonanti /p/ katika fonolojia ya Kiarror na haiwezi kutokea katika mazingira ya kutanguliwa na kufuatwa moja kwa moja na irabu, yaani haiwezi kutumiwa kuunda silabi yenye muundo wa KI kama ilivyo katika Kiswahili, ila konsonanti /p/ katika Kiarror huweza kutumiwa katika mazingira kama hayo. Konsonanti /b/ katika Kiarror huweza tu kutumiwa pamoja na nazali /m/ katika kuunda konsonanti nazalishi /mb/, kama vile katika neno /sɛ**mb**er/ (palilia). Hivyo basi, Kiarror kinapokopa maneno ya Kiswahili yaliyo na konsonanti /b/ inayounda silabi ya KI, huibadilisha konsonanti hiyo kuwa /p/ kwa vile /b/ na /p/ zina uhusiano wa karibu wa kifonetiki kwa vile zote zinatamkiwa midomoni.

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (47 a) /**b**ata/ | /**p**ata/ |
| (47 b) /**b**unduki/ | /**p**unduki/ |
| (47 c) /**b**ara**b**ara/ | /**p**ara**p**ara/ |

/b/ ⟶ [p] / __ [irabu]

**(c) Kuimarika kwa /g/ kuwa /k/**

Konsonanti /g/ na /k/ ni vipasuo vya kaakaa laini kwa hivyo zina ukuruba wa karibu wa kifonetiki. Tofauti ni kwamba /g/ ni konsonanti ghuna ila /k/ ni konsonanti isoghuna. Konsonanti ghuna ya kaakaa laini /g/ huwa alofoni ya konsonanti /k/ katika Kiarror na hutokea tu ikiwa imeambatishwa na nazali /ɳ/ kama vile katika neno /soɳgo:i/ (bɛmbɛa) bali haitokei kama konsonanti inayojisimamia katika neno kama ilivyo katika Kiswahili, yaani haiwezi kuunda silabi yenye muundo wa KI. Kwa hivyo, neno la Kiswahili lililo na konsonanti /g/ linapokopwa na Kiarror, ni sharti konsonanti hiyo /g/ ibadilishwa kuwa /k/ ili neno lenyewe likubalike katika mofofonolojia ya Kiarror.

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (48 a) /**g**azɛti/ | /**k**asɛ:ti/ |
| (48 b) /**g**ari/ | /**k**ari/ |

(48 c) /**g**ilasi/ /**k**ila:si/

/g/ → [k] / __ /i/

Kanuni jumuishi kwenye mifanyiko hii ni:

$$\begin{bmatrix} \text{+kons} \\ \text{+kip} \\ \text{+mgh} \end{bmatrix} \rightarrow \begin{bmatrix} \text{+kons} \\ \text{+kip} \\ \text{-mgh} \end{bmatrix} \Big/ __ \begin{bmatrix} \text{+sila} \\ \text{-kons} \end{bmatrix}$$

**(iv) Kikwamizo (+ghuna) kubadilika kuwa kikwamizo (-ghuna)**

Konsonanti zinazohusishwa hapa ni /z/ na /s/ ambazo ni vikwamizo vya ufizi. Ingawa vikwamizo hivi hutofautiana kwa vile /z/ ni sauti ghuna nayo /s/ ni sauti isoghuna, konsonanti hizi mbili zina ukuruba mkubwa wa kifonetiki. Fonolojia ya Kiarror haina konsonanti /z/ ila fonolojia ya Kiswahili inayo. Kwa hivyo nomino za Kiswahili zilizo na konsonanti /z/ zikikopwa na Kiarror, ni sharti konsonanti hiyo itafutiwe kibadala kilicho kwenye fonolojia ya Kiarror ili neno liweze kukubalika katika Kiarror na kibadala chake kitakuwa konsonanti /s/ iliyo na ukuruba mkubwa zaidi kifonetiki na /z/. Kwa mfano:

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (49 a) /mɛ**z**a/ | /mɛ**s**a/ |
| (49 b) /via**z**i/ | /pia**s**i/ |
| (49 c) /ka**z**i/ | /ka**s**i/ |

/z/ → /s/ / __ [irabu]

Kanuni ya mfanyiko huu ni:

$$\begin{bmatrix} +\text{kons} \\ +\text{kmz} \\ +\text{ufz} \\ +\text{mgh} \end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix} +\text{kons} \\ +\text{kmz} \\ +\text{ufz} \\ -\text{mgh} \end{bmatrix} \Big/ \; __ \begin{bmatrix} +\text{sila} \\ -\text{kons} \end{bmatrix}$$

**(v) Kipasuo kwamizo (+ghuna) kuwa kipasuo kwamizo (-ghuna)**

Kipasuo kwamizo chenye mghuno /Ɉ/ cha kaakaa gumu hubadilishwa kuwa kipasuo kwamizo kisichoghuna /ʧ/ cha kaakaa gumu. Hali hii inatokea kwa sababu mfumo wa kifonolojia wa Kiarror hauna konsonanti /Ɉ/. Kifonetiki, /ʧ/ na /Ɉ/ ni konsonanti zilizo na ukuruba mkubwa kwani zote ni vipasuo kwamizwa na zote zinatamkiwa katika kaakaa gumu. Kwa hivyo maneno ya Kiswahili yanapokopwa na Kiarror, mchakato wa utohozi huhusisha kubadilisha /Ɉ/ kuwa /ʧ/ ili ikubalike katika mfumo wa Kiarror.

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (50 a) /ki**Ɉ**ikɔ/ | /kiʧi:kɔ/ |
| (50 b) /**Ɉ**umamɔsi/ | /ʧumɔmɔ:s/ |
| (50 c) /**Ɉ**ɛmbɛ/ | /ʧɛ:mbɛ/ |

/Ɉ/ ⟶ /ʧ/ / __ [irabu]

Kanuni ya mfanyiko huu ni:

$$\begin{bmatrix} +\text{kons} \\ +\text{kip kmz} \\ +\text{kk gumu} \\ +\text{mgh} \end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix} +\text{kons} \\ +\text{kip kmz} \\ +\text{kk gumu} \\ +\text{mgh} \end{bmatrix} \Big/ \; __ \begin{bmatrix} +\text{sila} \\ -\text{kons} \end{bmatrix}$$

#### 3.3.1.2 Kudhoofika kwa konsonanti

Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa kudhoofika kwa fonimu hutokea wakati ambapo nguvu chache za misuli zinatiwa katika ala za sauti na msukumo mdogo wa mkondohewa hutumika katika kutamka alofoni kuliko kutamka fonimu yake. Hivi ni kusema kuwa fonimu hudhoofika ikiwa inatamkwa kwa urahisi kuliko ilvyotamkwa mwanzoni. Utafiti huu umebainisha kutokea kwa hali hii kama ifuatavyo:

**(i) Kipasuo (-ghuna) kubadilika kuwa kikwamizo (+ghuna)**

Katika Kiarror, konsonanti /k/ ikitokea katikati mwa neno, ikiwa inafuata irabu, hubadilika kuwa kikwamizo /γ/. Kwa mantiki hiyo, nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili hufuata mtindo uo huo ili ziweze kukubalika katika mfumo wa Kiarror. Hali hii inadhihirishwa na mifano ifuatayo:

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (51 a) /m**k**atɛ/ | /ma**γ**atja:n/ |
| (51 b) /wa**k**ili/ | /ɔ**γ**iljɔ:n/ |
| (51 c) /ki**k**ɔmbɛ/ | /ki**ɣ**ɔmbɛ/ |

$$/k/ \longrightarrow [\gamma] \;/\; __ \;[\text{irabu}]$$

Kanuni inayoeleza badiliko hili ni:

$$\begin{bmatrix} \text{+kons} \\ \text{+kip} \\ \text{+kklaini} \\ \text{-mgh} \end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix} \text{+kons} \\ \text{+kmz} \\ \text{+kklaini} \\ \text{+mgh} \end{bmatrix} \;/\; __ \begin{bmatrix} \text{+sila} \\ \text{-kons} \end{bmatrix}$$

### 3.3.2 Uchopekaji wa konsonanti

Baadhi ya maneno yanayokopwa na Kiarror kutoka Kiswahili hutoholewa kwa kuchopekwa fonimu za konsonanti mwishoni mwa neno. Kama ilivyoelezwa hapo mwanzo, Kiarror hupendelea

muundo wa silabi funge (KIK) tofauti na Kiswahili ambacho kinapendelea silabi wazi (KI). Kwa mantiki hiyo, Kiarror huchopeka konsonanti mwishoni mwa maneno mkopo kutoka Kiswahili ili kuwe na muundo wa silabi funge mwishoni mwa neno husika. Hali kadhalika, kuna uchopezi mwingine utokeao kwa madhumuni ya kuunda viambishi vya umoja na wingi. Kwa mfano, katika nomino ya Kiswahili 'risasi', umoja wake katika Kiarror ni /risasjan/ na wingi wake ni /risasis/. Mifano ya maneno yanayohusishwa na mfanyiko huu ni:

/ø/ ⟶ [K] / /irabu/___

Mifano ya maneno yanayohusishwa na mifanyiko hii ni:

| **Kiswahili** | **Kiarror** | |
|---|---|---|
| | **Umoja** | **wingi** |
| (53 c) /fundi/ | /pundijɔ:**n/** | /pundi:**s** |
| (53 d) /taa/ | /tae**t**/ | /taeti**s**/ |
| (53 c) /daktari/ | /tɔktɔri**n**/ | /tɔktɔri**s**/ |

Mifanyiko hii ya uchopekaji huweza kuwakilishwa na kanuni jumuishi ifuatayo:

### 3.3.3 Udondoshaji wa konsonanti

Kiarror hudondosha konsonanti kutoka baadhi ya nomino mkopo kutoka Kiswahili. Aghalabu, konsonanti zinazodondoshwa ni zile zisizopatikana katika mfumo wa kifonolojia wa Kiarror. Nafasi ya konsonanti inayodondoshwa huweza kuachwa wazi au kuchukuliwa na fonimu nyingine.

#### (i) Udondoshaji wa konsonanti /h/

Utafiti huu ulibainisha kwamba konsonanti /h/ haipo katika mfumo wa kifonolojia wa Kiarror. Kwa mantiki hiyo, Kiarror kinapokopa nomino zenye konsonanti /h/, kinadondosha konsonanti hiyo ili kuifanya nomino ikubalike katika mfumo wa Kiarror. Konsonanti /h/ huweza kudondoshwa inapotokea mwanzoni mwa nomino mkopo kama ifuatavyo:

/h/ ⟶ [ø] / #___ /irabu/

Mifano ya nomino zinazoonyesha mfanyiko huu ni:

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (54 a) /**h**ɛma/ | /ɛ:ma/ |
| (54 b) /**h**ɛsabu/ | /ɛsa:pɔ/ |
| (54 c) /**h**abari/ | /apa:ri/ |

Mfanyiko huu unaweza kuwakilishwa na kanuni ifuatayo:

$$\begin{bmatrix} \text{+kons} \\ \text{+ kmz} \\ \text{+glt} \\ \text{-naz} \\ \text{-mgh} \end{bmatrix} \longrightarrow [\text{ø}] \; / \; \#___ \begin{bmatrix} \text{+sila} \\ \text{-kons} \end{bmatrix}$$

Konsonanti /h/ pia huweza kudondoshwa katikati mwa nomino mkopo kama ifuatavyo:

$$/\text{h}/ \longrightarrow [\text{ø}] \; / \; __ \; /\text{i}/$$

Mifano ya nomino zinazoonyesha mfanyiko huu ni:

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (54 c) /ru**h**usa/ | /rusa/ |
| (54 d) /mʃa**h**ara/ | /musjara/ |
| (54 e) /sa**h**ani/ | /sa:ni/ |
| (54 f) /ma**h**aragwɛ/ | /marakwa/ |

Mfanyiko huu unaweza kuwakilishwa na kanuni ifuatayo:

$$\begin{pmatrix} \text{+kons} \\ \text{+kmz} \\ \text{+glt} \\ \text{-naz} \\ \text{-mgh} \end{pmatrix} \longrightarrow [\text{ø}] \; / \; \begin{pmatrix} \text{+sila} \\ \text{-kons} \end{pmatrix} ___ \begin{pmatrix} \text{+sila} \\ \text{-kons} \end{pmatrix}$$

### 3.3.4 Ubadala wa konsonanti

Utafiti huu ulibainisha kuwa kuna mabadiliko ya konsonanti yasiyohusisha kudhoofika wala kuimarika kwa fonimu. Mabadiliko hayo ni yale ambayo hukumba konsonanti zinazotamkwa kwa kutumia kiasi sawa cha nguvu. Sababu ya kutukia kwa ubadala ni kupata konsonanti mbadala ya Kiarror hasa ikiwa neno linalokopwa kutoka Kiswahili lina konsonanti inayopatikana katika mfumo wa kifonolojia wa Kiswahili ila haipatikani katika mfumo wa Kiarror. Mifano ya konsonanti za Kiswahili ambazo hazipatikani katika mfumo wa Kiarror ni: /θ/, /ɟ/, /ʃ/, /ð/, /b/, /d/, /g/, /z/, /v/ na /f/. Mifano ifuatayo inadhihirisha ubadala.

**Konsonanti /ʃ/ kuwa /s/**

Katika mfanyiko huu, kikwamizo hafifu cha kaakaa gumu /ʃ/ hubadilishwa kuwa kikwamizo hafifu /s/ cha ufizi. Sababu ya tukio hili ni kwamba mfumo wa kifonolojia wa Kiarror hauna kikwamizo /ʃ/. Kwa hivyo, mchakato wa utohozi huibadilisha /ʃ/ kuwa sauti inayokaribiana nayo kifonetiki ambayo ni /s/ kwani ingawa zinatamkiwa sehemu tofauti, sauti hizi zote ni vikwamizo na ni hafifu. Mabadiliko haya hayahusishi kuimarika wala kudhoofika kwa konsonanti kwani zote kimatamshi hutumia kiasi sawa cha nguvu. Badiliko hili huisaidia Kiarror kuiziba pengo la ukosefu wa sauti /ʃ/ katika fonolojia yake katika harakati za kujiongezea msamiati. Mifano ifuatayo inadhihirisha hali hii:

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (56 a) /**ʃ**ɛrɛhɛ/ | /**s**ɛrɛ:/ |
| (56 b) /**ʃ**iliŋgi/ | /**s**iliŋ/ |
| (56 c) /mazi**ʃ**i/ | /masi**s**i/ |

/ʃ/ ⟶ [s] __ /i/

/θ/ ⟶ [s] /i/__/i/

$$\begin{bmatrix} +kons \\ +kmz \\ -mgh \\ +kkgumu \end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix} +kons \\ +kmz \\ -mgh \\ +ufz \end{bmatrix} \Big/ \;__\; \begin{bmatrix} +sila \\ -kons \end{bmatrix}$$

Utafiti huu vilevile ulibaini kuwa uyeyushaji hutokea katika baadhi ya maneno katika mchakato wa utohozi wa /ʃ/. Konsonanti /ʃ/ hubadilika kuwa /sj/. Hii hutokea /ʃ/ ikitangulia irabu /a/ katika neno, kwa mfano:

| **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|
| (56 d) /m**ʃ**ahara/ | /mu**sj**ara/ |
| (56 e) /diri**ʃ**a/ | /tIre:**sj**a/ |
| (56 f) /**ʃ**amba/ | /**sj**amba/ |

### 3.4 Utohozi wa silabi

Kutokana na ufafanuzi uliotolewa katika sura ya pili kuhusu muundo wa silabi za Kiarror na za Kiswahili, ilibainika kuwa Kiswahili kinapendelea silabi wazi (KI) ilhali Kiarror hupendelea silabi funge (KIK). Mchakato wa utohozi wa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili huweza kuhusisha kubadilishwa kwa miundo ya silabi. Aidha, ili maneno yakubalike katika mfumo wa kimofofonolojia wa Kiarror, ni sharti silabi zidondoshwe katika baadhi nomino mkopo na zingine

zichopekwe katika baadhi ya nomino mkopo. Michakato ya udondoshaji na uchopekaji wa silabi katika nomino mkopo imeelezwa katika sehemu zifuatazo.

### 3.4.1 Udondoshaji wa silabi

Utohozi wa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili hujumuisha udondoshaji wa fonimu na udondoshaji wa silabi. Utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili hutoholewa kwa kuzidondosha silabi za katikati mwa neno zilizo na konsonanti /h/. Hali hii inadhihirishwa na nomino zifuatazo:

| | **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|---|
| (57 a) | /ru**hu**sa/ | /rosa/ |
| (57 b) | /ma**ha**ragwɛ/ | /mara:kwa/ |
| (57 c) | /ba**ha**ʃa/ | /pa:sja/ |
| (57 d) | /sa**ha**ni/ | /sa:ni/ |

Katika mifano iliyotolewa hapo juu, silabi za Kiswahili zilizonukuliwa kwa herufi nzito ndizo zinazodondoshwa katika mchakato wa utohozi. Kanuni inayotawala udondoshaji huu ni kwamba silabi ya pili kutoka mwisho wa nomino mkopo hudondoshwa ikiwa silabi hiyo imeundwa kutokana na kikwamizo cha koromeo /h/ pamoja na irabu. Hali hii inatokea kwa sababu mfumo wa kifonolojia wa Kiarror hauna sauti /h/ ambayo hupatikana katika mfumo wa kifonolojia wa Kiswahili.

### 3.4.2 Uchopekaji wa silabi

Uchopekaji wa silabi hufanyika mara nyingi katika utohozi wa nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili kwa madhumuni ya kubainisha nomino katika umoja na wingi na wakati uo huo kuibua muundo wa silabi funge unaopendelewa na Kiarror. Uchopekaji wa silabi hujumuisha kuingizwa kwa irabu au konsonanti katika mazingira maalum ya kifonetiki. Kuna aina mbili za uchopekaji katika nomino mkopo za Kiarror; uchopekaji unaotokea katikati mwa neno na ule unaotokea mwishoni mwa neno. Aghalabu uchopekaji wa irabu hutokea katikati mwa neno nao uchopekaji wa konsonanti hutokea mwishoni mwa nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili. Aina hizi za uchopekaji zinadhihirika katika mifano ifuatayo:

**(i) Usilabishaji kupitia uchopekaji wa irabu**

Katika Kiarror, mwambatano wa konsonanti mwanzoni mwa nomino haupendelewi sana katika utamkaji jinsi ilivyo katika Kiswahili. Kwa sababu hiyo, wasemaji wa Kiarror wanapokumbana na nomino mkopo iliyo na mwambatano wa aina hiyo, hujaribu kutafuta njia ya kurahisisha utamkaji wake kwa kuchopeka irabu kati ya konsonanti husika. Mifano ifuatayo inadhihirisha hali hii:

| | **Kiswahili** | **Kiaarror** |
|---|---|---|
| (60 a) | /mkɔba/ | /**mɔ**kupɔ/ |
| (60 b) | /mʧɛlɛ/ | /**mu**ʧɛlɛ/ |
| (60 c) | /msumɛnɔ/ | /**mu**sumɛnɔ/ |
| (60 d) | /mkɔɳgɛ/ | /**mɔ**kɔ:ɳ/ |
| (60 e) | /stima/ | /**se**tema/ |
| (60 f) | /mtihani/ | /**mu**tjani/ |

Mifano iliyoonyeshwa hapo juu inadhihirisha uchopekaji wa irabu /ɔ/, /i/, /u/ na /ɛ/. Utaratibu huu umetokea ili kuepuka mwambatano wa konsonanti kama vile /mʃ/, /mk/, /mʧ/, /ms/ na /mt/.

**(ii) Usilabishaji kupitia uchopekaji wa konsonanti**

Kwa vile Kiarror hupendelea silabi funge, nomino mkopo kutoka Kiswahili zilizo na silabi wazi mwishoni huongezwa konsonanti mwishoni ili kuunda silabi funge kama katika mifano ifuatayo:

| | **Kiswahili** | **Kiarror** |
|---|---|---|
| (61 a) | /fundi/ | /pundi**jɔ:n**/ |
| (61 b) | /risasi/ | /risas**ja:n**/ |
| (61 c) | /mkɔra/ | /mukɔrɔ**jɔ:n**/ |
| (61 d) | /wakora/ | /mukɔr**ɔi:s**/ |
| (61 e) | /maʃiliɳgi/ | /siliɳgi:**s**/ |

Lengo la mabadiliko haya ni kufanya neno mkopo likubalike katika mfumo wa kimofofonolojia wa Kiarror. Konsonanti zinazoongezwa kwa nomino aghalabu huwa /n/, /s/ na /t/ ambazo hutumika kama koda za silabi za mwisho.

### 3.5 Hitimisho

Sura hii imefafanua mifanyiko ya kifonolojia katika utohozi wa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili. Utafiti wetu umedhihirisha kuwa sababu kuu ya mabadiliko ya kifonolojia katika maneno ya Kiswahili yanayokopwa na Kiarror, ni tofauti katika miundo ya kifonolojia na ya kimofolojia kati ya Kiswahili na Kiarror. Ni sharti neno linalokopwa litoholewe ili liweze kuafiki muundo wa lugha au lahaja inayokopa. Utohozi huu unahusisha mifanyiko ya konsonanti, irabu na silabi zinazounda maneno yanayokopwa na Kiarror kutoka Kiswahili. Mifanyiko ya irabu ni kama vile uchopekaji wa irabu, udondoshaji wa irabu, uwiano wa irabu na uyeyushaji. Mifanyiko ya konsonanti ni kama vile kuimarika na kudhoofika kwa konsonanti, uchopekaji wa konsonanti, udondoshaji wa konsonanti na ubadala wa konsonanti. Vilevile, ilibainika kuwa utaratibu wa utohozi hujumuisha kudondoshwa kwa silabi au kuongezwa kwa silabi katika maneno mkopo. Kanuni za mifanyiko hii zilielezwa kwa kutumia nadharia ya fonolojia zalishi asilia.

## SURA YA NNE

## UTOHOZI KIMOFOLOJIA WA MANENO MKOPO YA KIARROR KUTOKA KISWAHILI

### 4.0 Utangulizi

Katika sura ya tatu, tulichanganua taratibu za utohozi wa kifonolojia wa maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili. Sura hii ilichanganua namna ambavyo maneno mkopo ya Kiarror kutoka Kiswahili hutoholewa kimofolojia ili yaweze kukubalika katika mfumo wa kimofofonolojia wa Kiarror. Hata hivyo, si rahisi kuzielewa taratibu za kiutohozi wa kimofolojia katika maneno mkopo pasipokuwa na ufafanuzi wa vipengele vya kimofolojia vya lugha hiyo. Hivyo basi, tutaanza kwa kufafanua kimukhtasari vipengele vya kimofolojia vya Kiswahili na Kiarror. Ufafanuzi huo ulisaidia katika kudhihirisha tofauti zilizopo baina ya mifumo ya kimofolojia ya Kiarror na Kiswahili.

### 4.1 Mofolojia ya nomino za Kiswahili

Hali mbalimbali za nomino za Kiswahili kama vile ngeli, idadi, ukubwa na udogo hubainishwa kwa kutumia viambishi awali tofauti na nomino za Kiarror ambazo hazina makundi yanayotokana na viambishi awali. Kiswahili hutambulisha na kuzipanga nomino zake katika ngeli zinazobainishwa kwa kutumia viambishi awali. Uchunguzi huu unafanywa kwa kuzingatia uainishaji wa kimofolojia kwa vile ni uchunguzi wa kimofofonolojia na kinachozingatiwa ni maumbo ya nomino.

Ngeli za nomino za Kiswahili zimeainishwa na wataalamu mbalimbali kama vile Waihiga (1999) aliyeainisha nomino za Kiswahili katika ngeli nane. Mgullu (1999) anaainisha nomino za Kiswahili katika ngeli tisa, nao Habwe na Karanja (2004) wanaainisha nomino za Kiswahili katika ngeli kumi na nane kwa kutumia nambari pamoja na viambishi. Katika uainishaji huu, kila kiambishi ngeli kinapewa nambari ya kukitambulisha kwa mfano ngeli ya saba huchukua nomino zenye kiambishi {ki} kama vile neno [kitabu] kisha ngeli ya nane huwakilisha wingi wa ngeli ya saba na kiambishi chake ni {vi} kama vile katika neno [vitabu].

Uainishaji wa nomino za Kiswahili katika ngeli huwa tofauti na uainishaji wa nomino za Kiarror kwa sababu Kiswahili ni lugha ya kibantu iliyo na mfumo tofauti wa kimofolojia ikilinganishwa na Kiarror ambayo ni kinailoti. Nomino za Kiarror hazina makundi yanayotokana na viambishi awali vya nomino bali hutumia viambishi tamati katika kuainisha nomino zake.

## 4.2 Uainishaji wa nomino za Kiarror

Mofolojia ya nomino katika lugha za Kikalenjin huwa changamano na maelezo mbalimbali yametolewa na wanaisimu kama vile Toweett (1975) na Jerono (2011). Toweett (1975) aliainisha nomino za Kikalenjin katika aina kumi na moja; sita za umoja na tano za wingi. Katika uchunguzi wetu, tumebainisha aina sita za nomino za Kiarror kwa kuzingatia viambishi tamati vya hali ya wingi. Jerono (2011) anaeleza kuwa nomino za Kitugen huambishwa mwishoni katika kudhihirisha idadi ya nomino na kubainisha maumbo ya upili ya nomino. Nomino za Kiarror hudhihirisha maumbo mawili; umbo la msingi na umbo la upili.

Nomino zenye umbo la upili huwa nomino dhahiri au zinazorejelea vitu au hali mahususi mathalan nomino ambazo zimetajwa awali. Nomino hizi hutumika katika hali ambapo kile kinachotajwa na mzungumzaji kinafahamika kwa mzungumziwa. Kwa upande mwingine, nomino zenye umbo msingi ni nomino zisizo dhahiri au zinazorejelea vitu au hali zisizokuwa mahususi. Nomino hizi hutokea katika hali ambapo mzungumziwa hana ufahamu wa awali wa kile kinachotajwa na mzungumzaji. Utafiti huu utaainisha nomino za Kiarror, ambayo ni lahaja ya Kitugen, kulingana na viambishi tamati vya idadi na maumbo ya upili ya nomino. Utazingatia jinsi nomino za aina mbalimbali huweza kuchukua maumbo tofauti tofauti ya viambishi tamati ili kuonyesha umoja, wingi au umbo la upili la nomino.

### 4.2.1 Nomino za Kiarror katika umbo la msingi

Nomino za Kiarror katika umbo la msingi huchukua viambishi mbalimbali kwenye hali za umoja na wingi. Kuna nomino zinazochukua viambishi vya umoja lakini katika wingi hazichukui viambishi vyovyote. Maumbo ya wingi katika nomino hizo huwa ndiyo mizizi ya nomino husika. Aidha, kuna nomino zinazochukua viambishi vya wingi pekee. Nomino za aina hii katika umoja huwa mizizi. Kunazo pia nomino za Kiarror ambazo huchukua viambishi tamati vya umoja na wingi. Mwisho, kuna nomino za Kiarror ambazo hazichukui viambishi vyovyote ama katika umoja

au katika wingi. Sehemu hii itachanganua kategoria hizi nne za nomino katika maumbo yao ya msingi.

### 4.2.1.1 Nomino zinazochukua viambishi vya umoja pekee

Aina ya kwanza ya nomino za Kiarror inajumuisha zile nomino ambazo huwa na viambishi vya umoja lakini hazina viambishi vya wingi. Nomino za aina hii zikiwekwa katika hali ya wingi, viambishi vinavyobainisha umoja hudondoshwa kisha mzizi unaobakia unakuwa ndio wingi wa nomino husika. Viambishi vinavyotumiwa kubainisha umoja wa nomino hizi ni kama vile {ja:n}, {jɔ:n} kama ifuatavyo:

| | Umoja | Kiambishi cha umoja | Wingi | Maana |
|---|---|---|---|---|
| (62 a) | [mɔrja:n] | {a:n} | [mɔr] | panya |
| (62 b) | [sɛɣɛmja:n] | {a:n} | [sɛɣɛm] | nyuki |
| (62 c) | [tɔritjɔ:n] | {ɔ:n} | [tɔri:t] | ndege |

Vile vile, kiambishi {at} huambishwa mwishoni mwa nomino za Kiarror ili kudhihirisha umoja. Hata hivyo, ni nomino chache zinazotumia kiambishi {at} kuonyesha umoja, kama vile:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (62 d) | [kɔɣɛ:lat] | {at} | [kɔɣɛ:l] | nyota |
| (62 e) | [kalja:ɳat] | {at} | [kalja:ɳ] | nzi |
| (62 f) | [pɛ:rat] | {at} | [pɛ:r] | ganda |

Kiambishi kingine kinachotumiwa kudhihirisha umoja wa nomino ni kiambishi {i:n}. Kiambishi {i:n} hutumika kudhihirisha umoja wa nomino zinazoundwa kutokana na vitenzi kama vile katika mfano (62 g), nomino [ʧori:n] ‘mwizi’ imeundwa kutokana na kitenzi [ʧɔ:r] ‘iba’.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (62 g) | [ʧori:n] | {i:n] | [ʧo:r] | mwizi |
| (62 h) | [kɔnɛti:n] | {i:n} | [kɔnɛ:t] | mwalimu |
| (62 i) | [kirwɔɣi:n] | {i:n} | [kirwɔ:k] | jaji |

Ikiwa mzizi unaishia irabu, mchakato wa uyeyushaji hufanyika ambapo irabu hiyo hubadilika kuwa kiyeyushi /j/ kama vile katika (62 i) na (62 k). Mfanyiko huu hutokea kwa sababu Kiarror hakiruhusu kufuatana kwa irabu tatu za aina moja katika neno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| (62 j) [lɔɣɔjɔ:n] | {jɔ:n} | [lɔɣɔi] | tunda |
| (62 k) [sumejɔ:n] | {jɔ:n} | [sumei] | unywele |
| (62 l) [sɔnɔjɔ:n] | {jɔ:n} | [sɔnɔi] | ushanga |

#### 4.2.1.2 Nomino zinazochukua viambishi vya wingi pekee

Kundi hili kinahusisha nomino ambazo katika umoja, zinadhihirika kama mizizi huru inayosheheni maana ya kileksika, yaani ni maneno mazima yanayojitegemea kimaana na kimuundo. Nomino hizi zikigeuzwa katika hali ya wingi ndipo viambishi tamati vinaongezwa. Nomino za aina hii huwa nyingi katika Kiarror. Baadhi viambishi tamati vinavyodhihirisha wingi ni {ɔ:n}, {ɛ:n}, {in} na {u:n} kwa mfano:

| | **Umoja** | **Wingi** | **Kiambishi cha wingi** | **Maana** |
|---|---|---|---|---|
| (63 a) | [sɔt] | [sɔtɔ:n] | {ɔ:n} | kibuyu |
| (63 b) | [lɔ:l] | [lɔ:lɔ:n] | {ɔ:n} | mfuko |
| (63 c) | [mɔ:] | [mɔ:n] | {ɔ:n} | tumbo |

Kwa vile Kiarror hakiruhusu kufuatana kwa irabu tatu mfululizo katika neno moja, mfano (63 c) wa neno [mɔ:] unahusisha kudondoshwa kwa irabu moja /ɔ/ katika wingi ili kuwe na [mɔ:n].

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (63 d) | [i:t] | [i:tin] | {in} | sikio |
| (63 e) | [ko] | [korin] | {in} | nyumba |

Katika (63 e), kimadende /r/ kimechopekwa kati ya irabu inayotamatisha mzizi na irabu inayotanguliza kiambishi cha idadi ili kubainisha maana ya kileksika ya neno.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (63 f) | [ser] | [seru:n] | {u:n} | pua |
| (63 g) | [ej] | [eun] | {un} | mkono |

Viambishi vingine vinavyotumiwa kuonyesha wingi wa nomino za Kiarror ni {ɔi}, na {oi} kwa mfano:

| | Umoja | Wingi | viambishi vya wingi | maana |
|---|---|---|---|---|
| (64 a) | [ɛrɛn] | [erenoi] | {oi} | nyoka |
| (64 b) | [ɳɛʧɛr] | [ɳeʧeroi] | {oi} | kiti |
| (64 c) | [ku:tuɳ] | [ku:tuɳɔi] | {ɔi} | goti |
| (64 d) | [ ɳgur] | [ɳgurɔi | {ɔi} | nguo |

Aidha, viambishi {wɔ} na {wɔk} hutumika kudhihirisha wingi. Maneno yanayotumia viambishi hivi huwa chache katika Kiarror, kwa mfano:

| | Umoja | wingi | viambishi vya wingi | maana |
|---|---|---|---|---|
| (65 a) | [teɳgek] | [teɳgekwɔ:k] | {wɔ:k} | dhambi |
| (65 b) | [tien] | [tienwɔ:k] | {wɔ:k} | wimbo |
| (65 c) | [po:r] | [po:rwɔ] | {wɔ} | mwili |
| (65 d) | [riɣei] | [riɣejwɔ] | {wɔ} | kamba |

Baadhi ya viambishi tamati vinavyoambishwa ili kudhihirisha wingi wa nomino ni {i:s}, {os} na {u:s} kwa mfano:

| | Umoja | Wingi | Kiambishi cha wingi | Maana |
|---|---|---|---|---|
| (63 a) | [suɣut] | [suɣuti:s] | {i:s} | ngoma |
| (63 b) | [taßo:t] | [taßo:ti:s] | {i:s} | dari |
| (63 c) | [kusjɔk] | [kusjɔɣu:s] | {u:s} | paa |
| (63 d) | [ko:t] | [ko:tos] | {os} | mdomo |

**4.2.1.3 Nomino zinazochukua viambishi idadi vya umoja na wingi**

Kikundi hiki kinajumuisha nomino zinazoambishwa viambishi tamati kuashiria umoja na wingi. Viambishi vya wingi huwa {en} na {ɔi}. Viambishi vya umoja huweza kuwa irabu au nusu irabu na irabu. Katika nomino ambazo mizizi yao huishia konsonanti za ufizi, viambishi tamati huwa nusu irabu pamoja na irabu.

| | Umoja | Kiambishi cha umoja | Wingi | Kiambishi cha wingi | Maana |
|---|---|---|---|---|---|
| (64 a) | [mɔ:rnɔ] | {ɔ} | [mɔ:ren] | {en} | kidole |
| (64 b) | [kɔi] | {i} | [koen] | {en} | jiwe |
| (64 c) | [keske] | {e} | [keske:n] | {en} | kiota |
| (64 d) | [ta:pta] | {a} | [ta:ptɔi] | {ɔi} | ua |
| (64 e) | [siɣirjɔ] | {jɔ} | [siɣirɔi] | {ɔi} | punda |
| (64 f) | [la:kwa] | {wa} | [la:ɣɔi] | {ɔi} | mtoto |

Katika (64 a) mpaka (64 c), viambishi vya umoja ni irabu na vya wingi ni {en}. Inabainika hapa kuwa nomino zilizo na irabu /ɔ/ au /e/ katika mzizi huambishwa kiambishi {en} cha umoja. Tukio hili linasababishwa kifonolojia ambapo kuna uwiano wa irabu ya mzizi na ya kiambishi. Nomino zilizo na kiambishi cha umoja kinachojumuisha nusu irabu na irabu hutumia {ɔi} kama kiambishi cha wingi kama katika (64 e) na (64 f).

#### 4.2.1.4 Nomino zisizochukua viambishi vya umoja wala vya wingi

Hizi ni nomino za kipekee ambazo hazichukui viambishi vyovyote aidha katika umoja au katika wingi. Nomino hizi huweza kutokea katika umoja pekee au katika wingi pekee. Kwa mfano, nomino katika (65 a) na (65 b) zinatokea katika umoja pekee, na (65 c) na (65 d) hutokea katika wingi pekee.

| | Nomino | Maana |
|---|---|---|
| (65 a) | [asi:s] | jua |
| (65 b) | [arawa] | mwezi |
| (65 d) | [pei] | maji |
| (65 e) | [ʧɛ] | maziwa |

Nomino hizi hazichukui viambishi vya umoja wala vya wingi.

### 4.2.2 Utohozi kimofolojia wa nomino mkopo katika umbo la msingi

Nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili zinapotoholewa, huchukua mfumo wa kimofolojia wa Kiarror. Lugha ya Kiswahili na Kiarror huwa na mifumo tofauti ya uambishaji idadi. Kwa mfano, mofimu za hali za umoja na wingi katika Kiswahili huambishwa kabla ya mzizi wa neno na katika Kiarror, mofimu za umoja na wingi huambishwa baada ya mzizi wa neno. Hivyo basi, nomino zikikopwa na Kiarror kutoka Kiswahili ni sharti zitoholewe ili zichukue viambishi tamati vinavyowakilisha mofimu za umoja na wingi, sawa na nomino nyinginezo zenye asili ya Kiarror.

#### 4.2.2.1 Nomino mkopo zinazochukua viambishi tamati vya wingi

Nyingi ya nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili huambishwa wingi pekee. Nomino hizi katika umoja huwa mizizi. Viambishi vya wingi vinavyotumiwa katika nomino mkopo ni {nɔi}, {nai}, na {s} kwa mfano:

| | Nomino | Wingi | Maana |
|---|---|---|---|
| (66 a) | [meli] | [melinɔi] | meli |
| (66 b) | [wembe] | [wembenɔi] | wembe |
| (66 c) | [ʧupɔ] | [ʧupɔnɔi] | chupa |
| (66 d) | [pasja] | [pasjanai] | bahasha |
| (66 e) | [kɔra] | [kɔranai] | kura |
| (66 f) | [ɛma] | [ɛmanai] | hema |

Nomino katika (66 a)- (66 c) hutumia kiambishi tamati cha wingi {nɔi} nazo nomino (66 d) – (66 e) hutumia kiambishi cha wingi {nai}. Matumizi ya kiambishi {nɔi} au {nai} husababishwa na uwiano wa irabu ambapo nomino ambazo huwa na mizizi inayoishia irabu /e/, /ɔ/ na /i/ huchukua kiambishi {nɔi} nazo nomino zilizo na mizizi inayoishia irabu /a/ huchukua kiambishi {nai}. Nomino zinazochukua viambishi {s} ni kama zifuatazo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (66 g) | [kilamɛt] | [kilamɛtis] | kalamu |
| (66 h) | [kasɛti] | [kasɛtis] | gazeti |

| | | | |
|---|---|---|---|
| (66 i] | [kitapɔ] | [kitapɔs] | kitabu |
| (66 j) | [kiʧikɔ] | [kiʧikɔs] | kijiko |
| (66 ) | [kiɣɔmbɛ] | [kiɣɔmbɛs] | kikombe |

Mifano hii inabainisha kuwa mizizi inayoishia irabu /i/, /ɔ/ au /ɛ/ huambishwa /s/ ili kudhihirisha wingi wa nomino isipokuwa katika (66 h) ambapo mzizi unaishia kipasuo cha ufizi /t/, kwa hivyo, kiambishi kinachopekwa irabu baina ya /t/ na /s/ ili kuvunja mfuatano wa kipasuo na kikwamizo cha ufizi; tukio ambalo mfumo wa Kiarror haukubali.

#### 4.2.2.2 Nomino mkopo zinazochukua viambishi tamati vya umoja

Kuna nomino mkopo, japo chache, zinazoambishwa katika umoja pekee. Nomino hizo katika wingi huwa mzizi. Katika umoja, nomino hizo huambishwa kiambishi {ja:n} au {jɔ:n} kwa sababu ya uwiano wa irabu za mwishoni mwa mzizi na za viambishi. Kwa mfano, mizizi inayoishia irabu /ɛ/ au /ɔ/ huchukua kiambishi {jɔ:n} nayo inayoishia irabu /a/ huchukua kiambishi {ja:n} kama ifuatavyo:

| | Umoja | Wingi | Maana |
|---|---|---|---|
| (67 a) | [maɛmbɛjɔ:n] | [maɛmbɛ] | embe |
| (67 b) | [pitɔjɔ:n] | [pitɔ] | fito |
| (67 c) | [kawaja:n] | [ka:wa] | mkahawa (mmea) |
| (67 d) | [pijasja:n] | [pijasi] | kiazi |

#### 4.2.2.3 Nomino mkopo zinazochukua viambishi tamati vya umoja na vya wingi

Kuna nomino mkopo zingine ambazo zinaambishwa katika umoja na katika wingi. Katika umoja, nomino hizi huchukua viambishi {jɔ:n} na {ja:n} na katika wingi, zinachukua kiambishi tamati {i:n} au {is} Kwa mfano:

| | Umoja | Wingi | Maana |
|---|---|---|---|
| (68 a) | [mɔɣɔjɔ:n] | [mɔɣɔi:n] | mhogo |
| (68 b) | [ndimɔjɔ:n] | [ndimɔi:n] | ndimu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| (68 c) | [ʧapatja:n] | [ʧapati:n] | chapati |
| (68 e) | [malaiɣaja:n] | [malaiɣai:s] | Malaika |

### 4.3 Nomino za upili

Nomino za Kiarror katika umbo la upili huambishwa mwishoni katika umoja na wingi. Viambishi tamati katika umbo la upili hutumiwa kubainisha nomino dhahiri. Katika sehemu hii, nomino za Kiarror katika umbo la upili zitabainishwa kwa kuzingatia viambishi tamati. Mifano itakayotumiwa ni ya aina tatu ambazo zimeelezwa hapo awali: Aina ya kwanza ni nomino zinazochukua viambishi vya umoja pekee. Aina ya pili itajumuisha nomino zinazochukua viambishi vya wingi pekee, ya tatu ni nomino zinazochukua vya umoja na wingi nayo ya nne ni nomino zisizochukua viambishi vyovyote.

#### 4.3.1 Nomino zinazochukua viambishi vya umoja

Viambishi tamati vinavyotumiwa katika umoja huwa {dɛ:}, {de:} na {ɛ:}. Katika wingi, viambishi {ik}, {ɛ:k} na {e:k} hutumika. Nomino zinazoishia nazali ya ufizi /n/ katika umoja huchukua kiambishi {dɛ} au {de} kama katika mifano ifuatayo.

| | **Umoja** | **Wingi** | **Maana** |
|---|---|---|---|
| (69 a) | [mɔrjandɛ:] | [mɔrɛ:k] | panya |
| (69 b) | [sɛɣɛmjandɛ:] | [sɛɣɛmik] | nyuki |
| (69 c) | [kɔnɛtinde:] | [kɔnɛ:tik] | mwalimu |
| (69 d) | [lɔɣɔjɔnde:] | [lɔɣɔɛ:k] | tunda |

Kwa upande mwingine, nomino zinazoishia kipasuo cha ufizi /t/ katika umoja huchukua kiambishi {ɛ}.

| | | | |
|---|---|---|---|
| (69 e) | [kɔɣɛ:latɛ:] | [kɔɣɛlɛ:k] | nyota |
| (69 f) | [kaljaɳatɛ:] | [kaljaɳɛ:k] | nzi |

Pia, ni wazi kuwa matukio haya ya uambishaji hufuata kanuni za kifonolojia. Kwa mfano, irabu inayojenga kiambishi huwiana na ile inayojenga mzizi. Nomino zenye irabu /a/ katika silabi ya

mwisho ya nomino ya umoja huchukua kiambishi {dɛ:} au {ɛ:}. Nomino zilizo na irabu /ɔ/ au /i/ katika silabi ya mwisho huchukua kiambishi {de}.

### 4.3.2 Nomino zinazoambishwa wingi

Nomino zinazoambishwa wingi zikiwa katika umbo la upili, huweza kuchukua kiambishi viambishi mbalimbali kutegemea miundo ya viambishi vya wingi. Kwa mfano, nomino zinazochukua kiambishi cha wingi {ɔ:n} huchukua kiambishi {ɛ:} au {e:} katika umoja na kiambishi {ik} katika wingi, kama vile:

| | **Umoja** | **Wingi** | **Maana** |
|---|---|---|---|
| (70 a) | [sote:] | [soto:nik] | kibuyu |
| (70 b) | [lɔlɛ:] | [lɔlɔ:nik] | mifuko |
| (70 c) | [mɔɛ:] | [mɔ:nik] | tumbo |

Nomino zilizo na kiambishi cha wingi kinachoishia /n/ huchukua kiambishi {ik} katika wingi. Kwa mfano:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (70 f) | [seru:] | [seru:nik] | pua |
| (70 g) | [eu:] | [eu:nik] | mkono |
| 0 d) | [iti:] | [i:ti:k] | sikio |
| (70 e) | [kɔ:t] | [kori:k] | nyumba |

Nomino zinazochukua kiambishi cha wingi {ɔi} zinapowekwa katika umbo la upili, huchukua kiambishi {k} katika wingi na {tɔ}, {je:} au {jɛ:} katika umoja kama ifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (70 h) | [ku:tuɳtɔ] | [ku:tuɳɔik] | goti |
| (70 ) | [ɳgurje:] | [ɳgurɔik] | nguo |
| (70 ) | [kimaɣɛ:tjɛ] | [kimaɣɛtɔik] | fisi |

Nomino zinazochukua kiambishi cha wingi {wɔk} zikiwekwa katika umbo la upili huambishwa {ik} katika wingi na {tɔ} katika umoja. Kwa mfano:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (70 i) | [teɳgektɔ] | [teɳgekwɔɣik] | dhambi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| (70 j) | [tiendɔ] | [tienwɔɣik] | wimbo |

Nomino zinazochukua kiambishi cha wingi {wɔ} zikiwekwa katika umbo la upili, irabu /ɔ/ hudondoshwa kisha /e:/ huchukua nafasi yake ili kuunda kiambishi {e:k} kwa mfano:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (70 k) | [po:rtɔ] | [porwe:k] | mwili |
| (70 l) | [riɣeitɔ] | [riɣeiwe:k] | Kamba |

### 4.3.3 Nomino zinazoambishwa umoja na wingi

Maumbo ya upili ya nomino zinazochukua viambishi vya umoja na vya wingi hudhihirishwa kwa kutumia kiambishi {k} katika wingi na {tɔ}, {e:} au {ɛ:} katika umoja.

| | **Umoja** | **wingi** | **maana** |
|---|---|---|---|
| (71 a) | [kɔitɔ] | [kɔɛ:k] | jiwe |
| (71 b) | [taptɛ:] | [taptɔik] | ua |
| (71 c) | [siɣirje:] | [sigirɔik] | punda |
| (71 d) | [mɔ:rne:] | [mɔ:re:k] | kidole |

Katika mfano (71 a) na (71 d), nazali ya ufizi /n/ inayotamatisha kiambishi cha wingi wa nomino katika umbo la msingi [kɔen] na [mɔ:ren] hudondoshwa kisha irabu /e/ hurefushwa ili kuunda kiambishi {e:k}.

### 4.3.4 Nomino zisizoambishwa umoja wala wingi

Viambishi vinavyodhihirisha umbo la upili katika nomino hizi ni {ta} na {ɛ:} ambavyo huwa viambishi vinavyotumiwa kudhihirishanumbo la upili katika nomino zilizo katika hali ya umoja, kama vile katika (72 a)- (72 c). Katika (72 d), kiambishi kinachodhihirisha umbo la upili ni {ɣɔ}.

| | **Nomino** | **Maana** |
|---|---|---|
| (72 a) | [asIsta] | jua |
| (72 b) | [arawɛ:] | mbalamwezi |
| (72 c) | [jɔmɛ:] | upepo |
| (72 d) | [ʧe:ɣɔ] | maziwa |

#### 4.3.5 Uambishaji wa nomino mkopo katika umbo la upili

Nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili huchukua mfumo wa Kiarror wa uambishaji tamati kudhihirisha umbo la upili la nomino.

##### 4.3.5.1 Nomino mkopo zinazochukua viambishi vya wingi pekee

Nomino mkopo za Kiarror kutoka kiswahili zinazochukua viambishi vya wingi pekee katika umbo la msingi huchukua kiambishi {k} au {jɛ:k} katika wingi ili kudhihirisha umbo la upili. Katika umoja, nomino hizi hudhihirisha umbo la upili kwa kurefusha irabu ya mwisho wa mzizi.

| | Umoja | Wingi | Maana |
|---|---|---|---|
| (73 a) | [meli:] | [meli:nɔik] | meli |
| (73 b) | [kari:] | [kari:nɔik] | gari |
| (73 c) | [ʧupɛ:] | [ʧupɔsjɛ:k] | chupa |
| (73 d) | [kɔrɛ:] | [kɔrasjɛ:k] | kura |

Mifano hii inadhihirisha kwamba nomino mkopo zinazochukua kiambishi {ɔi} huambishwa {k} mwishoni ili kudhihirisha umbo la upili. Nomino zinazochukua kiambishi tamati {s} huambishwa {jɛ:k} katika kudhihirisha umbo la upili.

##### 4.3.5.2 Nomino mkopo zinazochukua viambishi vya umoja pekee

Nomino zinazochukua viambishi vya umoja pekee katika umbo la msingi huchukua kiambishi {nde:} au {ndɛ:} katika umoja na {ik}, {ek} na {ɛk] katika wingi.

| | Umoja | Wingi | Maana |
|---|---|---|---|
| (74 a) | [maembejɔnde:] | [maembe:k] | embe |
| (74 b) | [pitɔjɔnde:] | [pite:k] | fito |
| (74 c) | [kawajandɛ:] | [kawɛ:k] | kahawa |
| (74 d) | [pijasjandɛ:] | [pijasi:k] | kiazi |

Mifano hii inadhihirisha kwamba nomino za umoja zilizo na irabu /e/ au /ɔ/ katika silabi ya mwisho ya mzizi katika umbo la msingi huchukua kiambishi {nde:} katika umbo la upili. Kwa upande

mwingine, nomino zilizo na irabu /a/ kwenye silabi ya mwisho wa mzizi katika umbo la msingi huchukua kiambishi {ndɛ:} katika umbo la upili. Katika wingi, uundaji wa nomino za umbo la upili huhusisha urefushaji wa irabu ya mwisho wa nomino katika umbo la msingi kisha kipasuo /k huchopekwa mwishoni. Kwa mfano katika [maembe], irabu /e/ imerefushwa kisha /k/ ikachopekwa mwishoni ili kuunda [maembe:k]. Katika (74 b) na (74 c), irabu ya mwisho /ɔ/ katika [pitɔ] na /a/ katika [kawa] hubadilishwa kuwa /e/ na /ɛ/ mtawalia ili /e/ iweze kuwiana na irabu /e/ inayounda kiambishi {ek} na /ɛ/ iwiane na irabu /ɛ/ inayounda kiambishi {ɛk}.

#### 4.3.5.3 Nomino mkopo zinazochukua viambishi vya umoja na vya wingi

Nomino zinazochukua viambishi vya umoja na vya wingi katika umbo la msingi zikigeuzwa katika umbo la upili huchukua kiambishi {de} au {dɛ} katika umoja na {ik} au {jɛ:k} katika wingi kama ifuatavyo:

| | **Umoja** | **Wingi** | **Maana** |
|---|---|---|---|
| (75 a) | [moɣojɔnde:] | [moɣoi:nik] | mhogo |
| (75 b) | [ndimɔjɔnde:] | [ndimɔi:nik] | ndimu |
| (75 c) | [ʧapatjandɛ:] | [ʧapati:nik] | chapati |
| (75 d) | [malaiɣajandɛ:] | [malaiɣaisjɛ:k] | Malaika |

Mifano hii inaonyesha kuwa nomino mkopo zinazochukua kiambishi cha wingi {is} huambishwa {jɛ:k} katika kudhihirisha umbo la upili. Nomino zinazochukua kiambishi cha wingi {i:n} huambishwa {ik}. Katika umoja, nomino mkopo zinazochukua kiambishi {jɔn} kwenye umbo la msingi huchukua kiambishi {de:} kwenye umbo la upili. Nomino zinazochukua kiambishi {jan} katika umbo la msingi huchukua kiambishi {dɛ} ili kuonyesha kuwa nomino inayorejelewa ni mahususi na inafahamika.

### 4.4 Mifanyiko ya kimofolojia ya utohozi wa nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili

Uchanganuzi wa mabadiliko ya kimofolojia katika nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili umebainisha kuwa utohozi wa wa nomino mkopo unahusisha uambishaji na unyambuaji. Kwa kiasi kikubwa, mchakato wa kimofolojia unaohusika katika utohozi huu ni uambishaji tamati. Aghalabu mofu za kudhihirisha idadi huambishwa mwishoni mwa nomino ili kubainisha umoja

na wingi. Wakati mwingine, nomino za umoja zisizo bayana huunda mizizi ya nomino kisha mofimu za wingi zinaambishwa mwishoni ili kuunda nomino za wingi. Kwa mfano:

| **Umoja (msi)** | **mofu umj (upi)** | **mofu wgi (msi)** | **mofu wgi (upi)** | **tafsiri** |
|---|---|---|---|---|
| (71 a) [taraʧ] | {ɛ:} | {i:s} | {isjɛ:k} | daraja |
| (71 b) [siliɳ] | {i:} | {i:s} | {isjɛ:k} | shilingi |
| (71 c) [ɳgur] | {je:} | {ɔi} | {ɔik} | nguo |
| (71 d) [kita:pɔ] | {ɔ} | {ɔs} | {ɔsjɛk} | vitabu |

Miundo mbalimbali ya nomino huzalishwa kutokana na mizizi inayokopwa kutoka Kiswahili. Kwa mfano, kutokana na nomino ‘daraja’, miundo ifuatayo ya nomino mkopo huweza kuzalishwa:

{taraʧ} + {ɛ:} > [taraʧɛ:] (daraja) (umj upi)

{taraʧ} + {is} > [taraʧi:s) (daraja) (wgi msi)

{taraʧ} + {isjɛk} > [taraʧisjɛ:k] (daraja) (wgi msi)

Kielelezo hiki kinathibitisha jinsi uambishaji tamati wa nomino mkopo kutoka Kiswahili kama mchakato wa kimofolojia unavyotokea katika Kiarror. Kutokana na kielelezo hiki, kanuni mbalimbali za kimofolojia zinaweza kubuniwa kama ifuatavyo:

Mzizi wa nomino (umj msi) + kiambishi (umj/wgi) > nomino

Kimsingi, utohozi wa kimofolojia wa nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili hufanyika kupitia mchakato wa uambishaji.

## 4.6 Hitimisho

Kijumla, imebainika kuwa nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili zinapotoholewa, huchukua mfumo wa kimofolojia wa Kiarror. Lugha ya Kiswahili na Kiarror huwa na mifumo tofauti ya uambishaji idadi. Mofimu za hali za umoja na wingi katika Kiswahili huambishwa kabla ya mzizi wa neno. Kwa upande mwingine, katika Kiarror, mofimu za umoja na wingi huambishwa baada ya mzizi wa neno. Hivyo basi, nomino mkopo zikitoholewa katika Kiarror zinachukua viambishi tamati vinavyowakilisha mofimu za umoja na wingi, sawa na nomino nyinginezo za kawaida za Kiarror. Sura hii imeangazia michakato ya kimofolojia inayohusishwa katika utohozi wa nomino za Kiswahili zinazoingizwa katika mfumo wa kimofolojia wa Kiarror. Uchunguzi umebainisha kuwa uambishaji ndio mchakato unaotumiwa pakubwa katika utaratibu wa utohozi. Uambishaji wa nomino za Kiarror kiidadi umeangaziwa kisha nomino mbalimbali za Kiswahili zikatambulishwa jinsi zinavoingizwa katika mfumo huo wa uambishaji. Aidha, tumeonyesha jinsi nomino mbalimbali zilizo na asili ya Kiarror na zinazokopwa kutoka Kiswahili zinavyoambishwa ili kudhihirisha maumbo yao ya upili. Kijumla, nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili hugeuzwa kimuundo ili ziweze kuafikiana na mfumo wa kimofolojia wa Kiarror.

## SURA YA TANO

## MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.0 Utangulizi

Sura hii itatoa itaangazia vipengele vitakavyohitimisha utafiti huu ambao madhumuni yake yalikuwa ni kuchanganua namna nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili zinavyotoholewa ili yaingizwe katika mfumo wa kifonolojia na wa kimofolojia wa Kiarror. Kwa kufanya hivyo, utafiti huu ulieleza sababu za mabadiliko mbalimbali ya kifonolojia na ya kimofolojia. Michakato ya kifonolojia na ya kimofolojia inayopitiwa na nomino mkopo katika harakati za utohozi ilifafanuliwa kwa kuzingatia Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia. Katika utafiti huu, tulilenga kubainisha kuwa nomino zinapokopwa na Kiarror kutoka Kiswahili hutoholewa kwa kuongozwa na mfumo wa kimofofonolojia wa Kiarror.

### 5.1 Mukhtasari wa matokeo

Katika utafiti huu, tulifafanua mfumo wa kifonolojia katika Kiarror na Kiswahili ambapo fonimu za Kiswahili na Kiarror ziliorodheshwa kwa madhumuni ya kubainisha tofauti za kifonolojia kati yao. Tofauti hizo za kifonolojia ndizo zinazosababisha mifanyiko ya kifonolojia wakati wa utohozi wa nomino mkopo. Konsonanti za Kiarror zilibainika kuwa kumi na tisa pamoja na nusu irabu mbili na konsonanti nazalishi nne. Kwingineko, konsonanti za Kiswahili zilibainishwa kuwa ishirini na nne na nusu irabu mbili. Irabu tisa fupi na irabu tisa ndefu za Kiarror ziliorodheshwa nazo irabu tano za Kiswahili zikaorodheshwa. Kwa kila fonimu iliyotajwa, sifa zake bainifu zilifafanuliwa.

Mfumo wa silabi katika Kiswahili na Kiarror pia ulifafanuliwa kwa kina kwa vile mchakato wa utohozi wa nomino mkopo huathiriwa na mfumo wa silabi za lugha chanzi na lugha pokezi. Mara nyingi, utaratibu wa kutohoa nomino mkopo huhusu kubadilishwa kwa muundo wa nomino husika ili ioane na mfumo wa silabi za lugha pokezi. Utafiti ulibainisha kuwepo kwa usawa na tofauti baina ya miundo ya silabi za Kiswahili na za Kiarror. Mathalan, silabi pendwa katika Kiarror huwa silabi funge KIK ilhali silabi pendwa katika Kiswahili huwa silabi wazi KI. Maelezo kuhusu fonimu na silabi za Kiswahili na Kiarror yalitumiwa kuweka msingi wa mifanyiko ya kifonolojia katika utohozi wa nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili.

Katika sura ya tatu, utafiti huu ulichanganua utohozi wa kifonolojia wa nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili ulifafanuliwa. Mifanyiko ya kifonolojia inayohusika katika utohozi ilichanganuliwa kwa kina na kanuni za mifanyiko hiyo zikadhihirishwa kulingana wa nadharia ya fonolojia zalishi asilia. Mifanyiko ya konsonanti ni kama vile udondoshaji wa konsonanti, uchopekaji wa konsonanti, kuimarika na kudhoofika kwa konsonanti. Kwa kuzingatia irabu, mifanyiko kama vile uwiano wa irabu, udondoshaji wa irabu, uchopekaji wa irabu na uyeyushaji ni miongoni mwa mifanyiko iliyofafanuliwa.

Aidha, katika kuchanganua utohozi wa kifonolojia, utafiti huu pia ulizingatia utohozi wa silabi za nomino mkopo kama vile uchopekaji na udondoshaji wa silabi. Kwa mujibu wa utafiti huu, uchopekaji na udondoshaji wa silabi za nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili hufanyika ili kuepuka msururu wa aina fulani za fonimu. Sababu nyingine ya kubadilika kwa silabi ni kuepuka baadhi ya konsonanti zisizopatikana katika mfumo wa kifonolojia wa Kiarror kama vile konsonanti /h/. Muundo wa silabi za nomino mkopo pia hubadilika katika mchakato wa utohozi ili kuafikia muundo wa silabi funge unaopendelewa na Kiarror.

Utafiti huu ulibainisha kuwepo kwa tofauti katika uambishaji idadi katika nomino za Kiswahili na za Kiarror. Wakati Kiswahili kinatumia uambishaji mwanzo kubainisha umoja na wingi wa nomino zake, Kiarror kinatumia uambishaji tamati. Vile vile, Kiarror hutumia viambishi tamati kuonyesha nomino zinazofahamika katika muktadha mahususi. Utafiti vilevile ulichanganua utohozi wa kimofolojia wa nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili. Ilibainika kuwa utaratibu wa utohozi wa kimofolojia wa nomino mkopo huhusisha uambishaji. Viambishi tamati ndivyo vinavyotumika katika utohozi ambapo viambishi vinavyotumika huwa vile vinavyowakilisha umoja wa nomino, wingi wa nomino na udhahiri wa nomino. Katika utaratibu huu, viambishi idadi vya Kiswahili hupoteza maana au kudondoshwa kabisa kisha viambishi tamati vya Kiarror vinatumika.

### 5.2 Hitimisho

Kutokana na matokeo ya utafiti wetu, ilibainika kwamba Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ni nadharia toshelevu inayoweza kutumika katika kufafanua utohozi wa nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili. Nadharia hii iliweza kueleza uhusiano baina ya miundo ndani na miundo nje ya michakato mbalimbali ya kifonolojia na ya kimofolojia ambayo huhusika katika utohozi wa

nomino mkopo. Kwa vile Fonolojia Zalishi Asilia ni nadharia inayosisitiza uchunguzi wa lugha katika uasilia wake, basi ni nadharia faafu zaidi katika kueleza sababu za mabadiliko yanayotokea katika lugha asilia. Hivyo basi, Kiarror, kama lugha yoyote asilia, hutumia michakato mbalimbali ya kifonolojia na kimofolojia kama mbinu za kuzitohoa nomino mkopo.

## 5.3 Mapendekezo

Utafiti wetu ulijikita katika mofofonolojia ya utohozi wa nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili. Viwango vya kiisimu vilivyozingatiwa ni fonolojia na mofolojia pekee. Hata hivyo, utohozi wa viwango vingine vya kiisimu kama vile semantiki huweza kutokea. Kwa mantiki hiyo, tunapendekeza utafiti ufanywe kwa kuzingatia utohozi wa kisemantiki wa nomino mkopo za Kiarror kutoka Kiswahili.

Aidha, utafiti wetu ulibainisha kuwa ingawa mabadiliko hufanywa katika maneno ya Kiswahili ili yaweze kuchukua mfumo wa kifonolojia na wa kimofolojia wa Kiarror, bado kunabakia mfanano fulani kati ya umbo la neno la lugha kopeshi (Kiswahili) na umbo la neno la lugha pokezi (Kiarror). Hata hivyo utafiti huu haukushughulikia suala hilo. Ni pendekezo letu basi kuwa utafiti ufanywe ili kuweka wazi suala hili katika mkabala wa Mlinganuo Chanzi.

## MAREJELEO


Anderson, S.R (1985) Phonology in the Twentieth Century: Theories of Rules and Theories of Representations. The University of Chicago Press, Chicago

Boen, P. C. (2014) Loanwords in Nandi from English and Kiswahili Language. Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi

Bynon, T. (1977). Historical Linguistics. Newyork. Cambridge University Press.

Cherono, N. J (2018) Msamiati Mkopo Katika Kipsigis: Uchanganuzi wa Kimofofonemiki na Kiisimu Jami. Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Moi

Habwe na Karanja, (2004) Misingi ya Sarufi ya Kiswahili. Phoenix Publishers. Nairobi

Habwe, Matei na Nyonje, (2010) Darubini ya Isimujamii kwa shule na vyuo. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Hooper, J. (1976) An Introduction to Natural Generative Phonology. Newyork Academic Press

Iribemwangi, P. I. (2008) A synchronic Morphophonology of Standard Swahili. Unpublished PhD Thesis, University of Nairobi.

Jerono, P. (2011) Tugen Word Order: A Minimalist Perspective. Kocani: Egalite Publishers

Jerono, P. (2018) Tugen Noun Classification in Schroeder H &P. Jerono (eds) Nilo Saharan Issues and Perspectives Vol 30: 87-96 Rudiger Kopper Verlag

Kandagor, M. & Sawe, S. (2014) Resyllabification of Loan Words in Kalenjin Phonology katika Research on Humanities and Social Sciences Vol. 4 No. 6

Kang' Y (2010) Suprasegmental adaptation in Loanwords. Retrieved from www.elsevier.com/locate/lingua.

Kiango, J.G (1999) Matatizo ya Utohoaji Maneno Kama Mbinu ya Kukopa Istilahi Katika Lugha. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Tanzania

Kolongei, P.C (2017) Fonolojia Arudhi ya Nomino Mkopo za Kikeiyo kutoka Kiswahili. Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Langacker, R.W (1967) Language and its Structure: Some Fundamental Linguistic Concepts. Harcourt, Brace & World, Inc.

Lehman, W.P (1962) Historical Linguistics: An Introduction: Rinehart and Winston

Massamba, D. P. B (2011) Maendeleo katika Nadharia ya Fonolojia. Dar es Salaam. TUKI

Massamba, D. P. B (2012) Misingi ya Fonolojia. Dar es Salaam. TUKI

Mbaabu, I (1991) Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili. Nairobi: Longman Publishers

Mgullu, R. S (1999) Mtalaa wa Isimu. Longhorn Publishers

Mwaliwa, C.H (2000) Ulinganishi wa Mofofonolojia ya Kiswahili na Kidawida. Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa, Chuo kikuu cha Nairobi

Obuchi, S. M & Mukhwana, A (2015) Muundo wa Kiswahili: Ngazi na Vipengele. Nairobi. JKF

Odlin, T (1989). Language Transfer. Newyork. Cambridge University Press.

Robins, R. H (1980) General Linguistics: An Introductory Survey. Longman Inc. Newyork. USA

Schane, S. A (1973) Generative Phonology. Prentice Hall: Cambridge University Press

Scotton, C. M (1972) Contact Linguistics: Bilingual Encounters and Grammatical Outcomes. Oxford, Oxford University Press

Toweett, T (1975) Kalenjin nouns and their Classification with Notes on Phonology and a Noun List Appendix. Unpublished M A Thesis, University of Nairobi.

Wa Mberia, K (1981) The Consonants of Kitharaka. Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi

Wardhaugh, R (1972) Introduction to Linguistics: Mc Graw-Hill Book Company. Newyork

## KIAMBATISHO

## MANENO MKOPO YA KIARROR KUTOKA KISWAHILI

| | KISWAHILI | KIARROR | | |
|---|---|---|---|---|
| | | UNUKUZI KIOTHOGRAFIA | UNUKUZI KIFONETIKI | |
| | | | UMOJA | WINGI |
| 1 | Meza | Mesa | [mɛsa] | [mɛsɔ:s] |
| 2 | Gari | Kari | [kari] | [kari:nɔi] |
| 3 | Hema | Ema | [ɛ:ma] | [ɛ:manai] |
| 4 | Makaa | Makaa | [maɣaja:n] | [maɣa:] |
| 5 | Daktari | Toktoriin | [tɔktɔri:n] | [tɔktɔri:s] |
| 6 | Mkoba | Mokupo | [mɔɣupɔ] | [mɔɣupɔ:s] |
| 7 | Mpira | Mbira | [mbira] | [mbira:nai] |
| 8 | Ndoo | Ndoit | [ndɔit] | [ndɔiti:s] |
| 9 | Ndizi | Ntisjon | [ntisjɔ:n] | [ntisi:n] |
| 10 | Kufuli | Kupuli | [kupuli] | [kupuli:s] |
| 11 | Panga | Panga | [paɳga] | [paɳgɛ:s] |
| 12 | Stima | Setema | [setema] | [setema:nai] |
| 13 | Simu | Simo | [si:mɔ] | [simɔ:nɔi] |
| 14 | Mali | Mali | [mali] | [mali] |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 15 | Lami | Lam | [la:m] | [lami:s] |
| 16 | Malaika | Malaikayan | [malaiɣaja:n] | [malaiɣai:s] |
| 17 | Chuma | Chumoyon | [ʧumɔjɔ:n] | [ʧumɔi:s] |
| 18 | Nyanya | Nyanyayan | [ɲaɲaja:n] | [ɲaɲa] |
| 19 | Nyundo | Nyundu | [ɲundu] | [ɲundu:s] |
| 20 | Yai | Mayayat | [majajat] | [majai] |
| 21 | Jela | Chela | [ʧɛla] | [ʧɛlanai] |
| 22 | Kijiko | Kichiko | [kiʧi:kɔ] | [kiʧikɔ:s] |
| 23 | Kikombe | Kikombe | [kiɣɔmbɛ] | [kiɣɔmbɛ:s] |
| 24 | Wembe | Wembe | [wembe] | [wembe:nɔi] |
| 25 | Kalamu | Kilaamet | [kila:met] | [kilamet:is] |
| 26 | Miwa | Mewayan | [mewaja:n] | [me:wa] |
| 27 | Kahawa | Kawayan | [kawaja:n] | [ka:wa] |
| 28 | Gazeti | Kaseeti | [kase:ti] | [kaseti:s] |
| 29 | Chai | Chai | | [ʧai] |
| 30 | Embe | Maembeyon | [maembejɔ:n] | [maembe] |
| 31 | Kipande | Kipandi | [kißandi] | [kißandi:s] |
| 32 | Karai | Karai | [karai] | [kɔrɔiwɔ] |
| 33 | Bahasha | Pasya | [pasja] | [pasja:nai] |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 34 | Bakuli | Pokuli | [pɔɣuli] | [pɔɣuli:s] |
| 35 | Baraza | Parasa | [para:sa] | [parasɛ:s] |
| 36 | Barua | Parwa | [parwa] | [parɔ:nɔi] |
| 37 | Bata | Pata | [pata] | [pata:nai] |
| 38 | Bendera | Pendera | [pɛndɛ:ra] | [pɛndɛrɛ:s] |
| 39 | Birika | Kipereka | [kißereɣa] | [kißerekai] |
| 40 | Chupa | Chupo | [ʧu:pɔ] | [ʧupɔ:nɔi] |
| 41 | Debe | Tepo | [te:pɔ] | [tepɔ:s] |
| 42 | Farasi | Paraasi | [para:si] | [parasi:s] |
| 43 | Firimbi | Pirimbi | [pirimbi] | [pirimbi:s] |
| 44 | Ghasia | Kasiya | [ɣasija] | [ɣasija] |
| 45 | Gitaa | Kitaa | [kita:] | [kitai:s] |
| 46 | Gunia | Koneya | [koneja] | [koneja:nai] |
| 47 | Jikoni | Chikoni | [ʧikɔ:ni] | [ʧikɔni:s] |
| 48 | Jumamosi | Chumomos | [ʧumɔmɔ:s] | [ʧumɔmɔsi:s] |
| 49 | Jumapili | Chumombili | [ʧumɔmbili] | [ʧumɔmbili:s] |
| 50 | Kalenda | Kalenda | [kalɛnda] | [kalɛndai:s] |
| 51 | Kamisi | Kamisi | [ka:misi] | [kamisi:s] |
| 52 | Kaputi | Kuputi | [kuputi] | [kuputi:s] |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 53 | Karatasi | Kartasi | [karta:si] | [kartasi:s] |
| 54 | Kikapu | Kikapo | [kiɣapɔ] | [kiɣapɔ:s] |
| 55 | Kinyozi | Kinyosi | [kiɲɔ:si] | [kiɲɔsi:s] |
| 56 | Kitabu | Kitapo | [kita:pɔ] | [kitapɔ:s] |
| 57 | Kitunguu | Kitunguuyon | [kituɳujɔ:n] | [kituɳui:s] |
| 58 | Kura | Kora | [kɔra] | [kɔra:nai] |
| 59 | Majani | Machani | [maʧa:ni] | [maʧa:ni] |
| 60 | Makasi | Makas | [maɣas] | [maɣasi:s] |
| 61 | Nanasi | Mananasyan | [mananasja:n] | [mananas] |
| 62 | Mpera | Maperayan | [mapɛraja:n] | [mapɛra] |
| 63 | Mchele | Muchelyon | [muʧɛljɔ:n] | [muʧɛ:lɛ] |
| 64 | Meli | Meli | [me:li] | [meli:nɔi] |
| 65 | Mhogo | Mokoyon | [mɔɣɔjɔ:n] | [mɔɣɔi:n] |
| 66 | Mkahawa | Makaw | [maɣaw] | [maɣawi:s] |
| 67 | Mkebe | Mekepe | [mɛɣɛpɛ] | [mɛɣɛpɛ:s] |
| 68 | Mkonge | Mokoong’ | [mɔɣɔ:ɳ] | [mɔɣɔɳgi:s] |
| 69 | Mshipi | Musipi | [musipi] | [musipi:s] |
| 70 | Msumeno | Musumeno | [musume:no] | [musumeno:s] |
| 71 | Mzabibu | Sapipchon | [sapipʧɔ:n] | [sapi:pu] |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 72 | Mzigo | Misiko | [misiɣɔ] | [misiɣɔ] |
| 73 | Ndege | Ndeke | [ndɛkɛ] | [ndɛɣɛnɔi] |
| 74 | Ndimu | Ndimoyon | [ndimɔjɔ:n] | [ndimɔi:n] |
| 75 | Ngumi | Ngumi | [ŋgumi] | [ŋgumi:nɔi] |
| 76 | Nguruwe | Ngurwee | [ŋgurwɛ:] | [ŋgurɔ:n] |
| 77 | Pasi | Paas | [pa:s] | [pasi:s] |
| 78 | Chumvi | Chumbi | | [ʧumbi] |
| 79 | Pikipiki | Pikipiki | [pikipiki] | [pikipiki:s] |
| 80 | Pingu | Pingoyoon | [piŋgɔjɔ:n] | [pingɔi:s] |
| 81 | Risasi | Risasyan | [risasja:n] | [risasi:s] |
| 82 | Ruhusa | Rosa | [rosa] | |
| 83 | Rungu | Rungu | [ruŋgu] | [ruŋgu:nɔi] |
| 84 | Sabuni | Supuni | [supuni] | [supuni:s] |
| 85 | Sadaka | Sataka | [sataka] | [sataka] |
| 86 | Safari | Sapari | [sapari] | [sapari:s] |
| 87 | Sahani | Saani | [sa:ni] | [sani:nɔi] |
| 88 | Serikali | Serkali | [serɣa:li] | [serɣali:s] |
| 89 | Siasa | Siasa | [siasa] | [siasa] |
| 90 | Sumu | Sumu | [sumu] | [sumu] |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 91 | Sururu | Sururu | [sururu] | [sururu:s] |
| 92 | Tarehe | Tarik | [tarik] | [tariki:s] |
| 93 | Wakili | Ogilyon | [ɔɣiljɔ:n] | [ɔɣilɔi] |
| 94 | Kibeti | Kipeti | [kipeti] | [kipeti:s] |
| 95 | Msalaba | Musalapa | [musala:pa] | [musalapa:nai] |
| 96 | Bunduki | Punduki | [punduɣi] | [punduɣi:s] |
| 97 | Baiskeli | Paskili | [paskili] | [paskili:s] |
| 98 | Kipindi | Kipindi | [kißindi] | [kißindi:s] |
| 99 | Kitana | Kipchanawa | [kipʧanawa] | [kipʧanawɛ:s] |
| 100 | Ufunguo | Kipunguu | [kipungu:] | [kipungui:s] |
| 101 | Redio | Retyo | [rɛtjɔ] | [rɛtjɔ:nɔi] |
| 102 | Kitambaa | Kitambaa | [kitambaa] | [kitambai:s] |
| 103 | Leso | Leso | [leso] | [leso:nɔi] |
| 104 | Sindano | Sendano | [sendanɔ] | [sendanɔ:s] |
| 105 | Mtaimbo | Tarimbo | [tari:mbɔ] | [tarimbɔ:nɔi] |
| 107 | Mbao | Paoyan | [paɔja:n] | [paɔwi:s] |
| 108 | Msumari | Kipchemaryan | [kipʧɛmarja:n] | [kipʧɛmari:s] |
| 109 | Ngazi | Ngaas | [ŋga:s] | [ŋgasi:s] |
| 110 | Taa | Taet | [taet] | [taeti:s] |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 111 | Kabati | Kapat | [kaßat] | [kaßatis] |
| 112 | Kiberiti | Kipiriti | [kißiriti] | [kißiriti:s] |
| 113 | Uma | Oma | [ɔ:ma] | [ɔma:nai] |
| 114 | Sufuria | Supuryo | [supurjɔ] | [supurɔi] |
| 115 | Sukari | Sakaro | | [saɣarɔ] |
| 116 | Viazi | Piyasyaan | [pijasja:n] | [pija:si] |
| 117 | Chapati | Chapatyaan | [ʧaßatja:n] | [ʧaßati:n] |
| 118 | Maharagwe | Marakwayaan | [marakwaja:n] | [marakwa] |